






## Wanafamilia mbaroni kwa tuhuma za mauaji

UKURASA 3



## RANGNICK: WASIO NA UWEZO KUONDOKA MANCHESTER UTD

UKURASA 21


# Nipashe

Jumanne Januari 25, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580836

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Kesi kupinga Ndugai kujiuzulu kunguruma

• **Itaanza** kesho Mahakama Kuu mbele ya jopo la majaji watatu... *Endelea ukurasa 2*



Mwenyekiti wa NCCR Mageuzi, James Mbatia (wapili kushoto), akizungumza na mawakili wake katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam jana, baada ya kufungua kesi ya kupinga mchakato wa kujiuzulu kwa aliyekuwa Spika wa Bunge, Job Ndugai. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### SHAHIDI AFUNGUKA KUWAKAMATA WALINZI WA MBOWE

SHAHIDI wa 11, Koplo Goodluck Minja amedai kuwakamata walinzi wa Mwenyekiti wa...

## Ummy: Marufuku kuitwisha mzigo Muhimbili

UKURASA 2



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani), jijini Dar es Salaam jana, kuhusu punguzo kubwa la riba katika mikopo ya kundi la wakulima. Wapili kulia ni Ofisa Mkuu wa Uendeshaji wa Benki ya CRBD, Bruce Mwile na Ofisa Mkuu wa Fedha, Fredrick Nshekanabo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Mjamzito na watoto wake wawili wachinjwa kinyama

UKURASA 2


**MICHEZO** **NABI AELEZA SIRI USHINDI YANGA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# HABARI KITAIFA



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akizungumza na wataalamu mkoani Tanga jana, kabla ya kikao kazi cha kujadili mikakati na kampeni ya kuhamasisha shughuli za ukuzaji viumbe maji baharini. Kulia kwake ni Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashim Mgandilwa. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

## Kesi kupinga kujiuzulu Ndugai kunguruma kesho

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam inatarajia kesho kuanza kusikiliza shauri la kikatiba la kupinga kujiuzulu kwa aliyekuwa Spika wa Bunge Job Ndugai na mchakato wa kupata mwingine kwa madai utaratibu ni batili.

Uamuzi huo wa Mahakama ulitolewa jana mbele ya jopo la majaji watatu wakiongozwa na Jaji John Mugeta.

Katika kesi hiyo iliyofunguliwa na Mwenyekiti wa NCCR-Mageuzi, James Mbatia, mdaiwa namba moja ni Job Ndugai, wapili ni Bunge na wa tatu ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mdaiwa wa pili na watatu wanawakilishwa na Mawakili Wakuu wa Serikali, Mussa Mbura, Deodatus Nyoni, Andrew Chang'a na Wakili wa Serikali, Stanley Kalokola.

Shauri hilo lilitakiwa kuanza kusikilizwa jana, lakini Ndugai hakuwapo wala wakili wake.

Wakili wa Serikali Mkuu, Mussa alidai shauri lilikuja kwa ajili ya kusikilizwa, lakini mdaiwa wa kwanza Ndugai hakuwapo na upande wa serikali haukuandaa majibu ya kiapo kinzani kwa sababu walipata taarifa jioni.

Wakili Mussa aliomba wapewe siku 14 ili wajibu na kwamba tukio la kujiuzulu Spika lilitokea Januari 6, mwaka huu na kesi ilifunguliwa Januari 21, walalamikaji Mbatia walipata muda wa siku 14 kuandaa kesi na hawaoni kama kuna dharura.

Wakili Mpare Mpoki akijibu, alidai dharura ipo kwa sababu kuna uchaguzi wa Spika wanauwahi, akichaguliwa mwingine kutakuwa na maspika wawili.

"Tunachoharakia uchaguzi wa Spika usifanyike, busara ya mahakama hii inatakiwa itoke kabla ya uchaguzi wa spika Januari 31, mwaka huu.

"Mahakama pekee ndiyo inayoweza kusimamisha uchaguzi wa Spika, hati ya wito waliyopewa serikali ilikuwa kesi inasikilizwa (leo) jana, hivyo walipaswa kuandaa majibu ya kiapo," alidai Mpoki.

Mahakama ilizingatia hoja na umuhimu wa suala lililoko mbele yake, ikaagiza mjibu maombi wa kwanza Ndugai apelekewe hati ya wito mkononi sio kwa email kama ilivyofanyika, kabla ya leo saa 8.30 mchana, majibu upande wa serikali yafike muda huo.

Jaji Mugeta aliahirisha shauri hilo hadi kesho kwa ajili ya kuanza kusikilizwa.

Mbatia anapinga utaratibu uliotumiwa na aliyekuwa Spika wa Bunge, Job Ndugai kujiuzulu na mchakato wa kupata spika mwingine.

Kesi hiyo ya kikatiba namba mbili ya mwaka 2022 ilifunguliwa chini ya hati ya dharura na inasikilizwa mbele ya jopo la majaji watatu.

"Katiba imeweka utaratibu, Spika akitaka kujiuzulu anatakiwa kwenda kufanya hivyo kwa watu waliomchagua ambao ni wabunge.

"Utaratibu uliotumiwa na Ndugai ni batili haukubaliki kikatiba," alidai Mbatia.

Mbatia anawakilishwa na jopo la mawakili 10 akiwamo Wakili Mpare Mpoki, Jeremiah Mtobesya.

Ndugai alijiuzulu uspika Januari 6, mwaka huu na Januari 21 mwaka huu, Dk. Tulia Ackson aliteuliwa kugombea nafasi hiyo.

## Mjamzito na watoto wake wachinjwa kinyama

**Na Gurian Adolf,**
SUMBAWANGA

MATUKIO ya mauaji yameendelea kwa kasi baada ya watu wasiojulikana kuua kwa kuchinja.

Kutokana na tukio hilo lilotokea Januari 17, mwaka huu, Jeshi la Polisi mkoani humo, limesema linawasaka watu hao kwa tuhuma za mauaji baada ya kutokomea kusikojulikana.

Jeshi hilo limesema tukio hilo linadhaniwa kutokea usiku wakati mama huyo na watoto wake wakiwa ndani ya nyumba yao, watu waliotekeleza mauaji hayo kuingia ndani.

Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Rukwa, Theopista Mallya, alisema mume wa mwanamke huyo ambaye yuko Dar es Salaam alianza kumtafuta mkewe Januari 21 kwa kumpigia simu, lakini ilikuwa inaita bila kupokelewa.

Alisema alipopiga kwa muda mrefu simu hiyo ilizima, hali inayoonyesha kuwa ilizima kwa kuishiwa chaji na kila alipojitahidi kupiga haikupatikana.

Baada ya hapo alimpigia rafiki yake, Paul Leonard, na kumwagiza aende akaione familia yake na alifika nyumbani hapo saa 2:30 usiku na alishangaa kukuta mlango umefungwa nje kwa kufuli, hivyo aliamua kuwaita viongozi wa kijiji na walipofika na kubomoa mlango na kuingia ndani walikuta mwanamke huyo aliyekuwa na ujauzito wa miezi minane akiwa amechinjwa pamoja na watoto wake Milliam (8) na William (4).

Mallya alisema wanatafuta ushahidi kwa kuwatafuta watu waliokuwa na mwanamke huyo kwa mara ya mwisho.

Katika toleo la jana Nipashe liliripoti watu watano wa familia moja, wakazi wa Kijiji cha Zanka wilayani Bahi mkoani Dodoma kuuawa kikatili na watu wasiojulikana huku miili yao ikikutwa ndani ya nyumba yao ikiwa imeanza kuharibika.

Waliouawa ni Hoseah Kapande ambaye ni baba wa familia hiyo na mkewe, Paulina Kapande. Wengine ni watoto wawili na mjukuu mmoja ambao ni Isack Kapande, mwanafunzi wa kidato cha kwanza, Agnes Kapande, mwanafunzi wa darasa la tatu na mjukuu aliyejulikana kwa jina la Heltony, mwanafunzi wa darasa la nne.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
25 – 01 - 2022

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumanne tarehe 25 – 01 – 2022** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd.** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Rufiji,** gari hizo zenye namba za usajili:
   **T 880 DXS / T 390 DHQ**
   **T 683 DUB / T 310 DDH**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 23**
   **Upana - mita 4.35**
   **Kimo - mita 5.00**
3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, Pwani hadi Rufiji kupitia Kibiti,** gari zitasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

216666102


## Marufuku kuitwisha mzigo Muhimbili

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amezipiga marufuku hospitali za kanda, rufani, mikoa na wilaya kuwahamishia wagonjwa wenye matatizo wanayoweza kuyatibu kwenda Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Agizo hilo alilitoa baada ya kutembelea MNH jana na kubaini kuwapo kwa mrundikano wa wagonjwa wanaotoka hospitali hizo kwa matatizo ya kawaida.

Akiwa katika kitengo cha dharura, alipokea malalamiko kutoka kwa watoa huduma ya kuwapo kwa mrundikano wa wagonjwa ambao miongoni mwao matatizo yanaweza kutibiwa walipotoka.

"Jambo ambalo limemleta ni la kuelemewa na idadi kubwa ya wagonjwa hapa MNH. Hospitali za wilaya, mkoa, rufani na kanda, nyingi hazitimizi wajibu wake ni lazima zitoe huduma bora ili kupunguza mzigo Muhimbili, inashangaza kuona hata mgonjwa ambaye hana damu anahamishiwa hapa huu ni uzembe," alisisitiza Ummy.

Alisema katika kukabiliana na mrundikano wa wagonjwa MNH hasa kitengo cha dharura, wanaandaa mpango mkakati wa kuboresha hospitali hiyo, iliyojengwa zaidi ya miaka 60 iliyopita ili iweze kudumu kwa miaka 50 ijayo.

"Tutaiboresha ili sasa iendane na wakati ulioko, haipendezi kuona wagonjwa wanalala kwenye kona na majengo yamechakaa," alisema Ummy.

Kadhalika alisema ipo haja ya kuwapo kwa Hospitali ya Kanda ya Dar es Salaam na Hospitali ya Taifa Muhimbili ili kupunguza mzigo wa wagonjwa kwa hospitali hiyo ya taifa.

Ummy pia alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa MHN, Prof. Lowrance Museru, kushughulikia changamoto alizopokea kutoka kwa wagonjwa kama kukaa wodini zaidi ya mwezi kusubiri matibabu.

Alitaja changamoto nyingine ni daktari kupita kwa awamu moja badala ya mbili, lugha mbaya kwa wagonjwa na kukosa huduma stahiki ilhali serikali imewekeza fedha za kutosha kuboresha mazingira na kuweka vifaa tiba vya kisasa.

Akijibu hoja za Ummy, Prof. Museru alisema katika kushughulikia lugha chafu kutoka kwa watumishi, tayari wametoa semina ya huduma kwa wateja kwa watoa huduma wa MNH na Mwananyamala na wanaendelea kufanya hivyo.

Prof. Museru alisema wagonjwa wanaokaa muda mrefu bila matibabu, wanakuwa wanaandaliwa kusubiri kufanyiwa upasuaji, na kuahidi kama kuna changamoto nyingine asizozifahamu atazifanyia kazi.

Kuhusu madaktari kupita mara moja, alisema daktari bingwa mmoja anapita mmoja ili kutoa maelekezo ya aina ya matibabu ya kupatiwa na awamu nyingine wanapita madaktari wa kawaida wakiwamo wanafunzi.

Alisema wanakabiliwa na changamoto ya wananchi kukimbilia kueleza kero zao kwenye mitandao ya kijamii, badala ya kutumia njia za kuwaona wahusika.

"Hili ni tatizo waziri, tuna hii shida mgonjwa hawezi kuja kulalamika anaenda kwenye mitandao kuandika na hata tunapotatua changamoto hawezi kurudi kusema alikosea anabaki kimya," alisema Prof. Museru.

**HABARI KITAIFA**

# Shahidi afunguka kuwakamata walinzi wa Freeman Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

SHAHIDI wa 11, Koplo Goodluck Minja amedai kuwakamata walinzi wa Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe kwa tuhuma za ugaidi haikuwa kumdhoofisha kisiasa wakati wa uchaguzi mkuu 2020.

Hayo yalidaiwa jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu mbele ya Jaji Joachim Tiganga wakati akihojiwa na Wakili wa Utetezi, Dickson Matata.

Matata alimuhoji akitaka kujua kama aliwahi kusikia Tundu Lissu kapigwa risasi 16 na kwamba alipigwa akiwa kwenye shughuli za Bunge.

Shahidi anadai aliwahi kusikia taarifa za Lissu kupigwa risasi Dodoma lakini hakuwahi kufuatilia.

Anadai hafahamu kati ya tukio la Lissu kupigwa risasi na tukio la kuwakamata watuhumiwa wa ugaidi Rau Madukani, Moshi kipi kilianza.

Shahidi anadai anafahamu kuwa Mbowe na Lissu ni viongozi wa CHADEMA na kwamba suala la Kiongozi kuwa na ulinzi wa mtu binafsi akiamua anakuwa naye.

Akihojiwa kuhusu suala la kuwakamata walinzi wa Mbowe haikuwa kumdhoofisha Mbowe wakati wa Uchaguzi 2020, alidai haikuwa na lengo la kumdhoofisha katika uchaguzi.

Koplo Goodluck anadai hafahamu Mbowe alikuwa mbunge wa wapi, lakini anafahamu alikuwa mbunge.

Akihojiwa na Wakili Peter Kibatala kuhusu mshtakiwa Adamu Kasekwa maarufu Adamoo alidai hakuna mahali ambapo alijitambulisha Adamoo na hakusikia kama alijitambulisha hivyo.

Anadai walipofika Dar es Salaam Agosti 7, mwaka 2020, wakiwa na mshtakiwa Kasekwa na Mohammed Ling'wenya alikwenda kunawa uso akiwa na vielelezo alivyowakamata navyo zikiwamo simu na bastola.

Anadai alikabidhi kwa Afande Nuru Agosti 7, mwaka 2020, lakini hakusema mahakamani kama risasi zilitolewa katika magazine wakahesabu.

Shahidi anadai mshtakiwa waliyemtafuta bila mafanikio Moshi, Moses alikuwa mwanajeshi lakini hakueleza mahakamani chochote kuhusu kushirikiana na jeshi liweze kusaidia.

Anadai hakueleza pia kuhusu kushirikiana na Interpol ili kumkamata mshtakiwa huyo.

Koplo Goodluck anadai anafahamu shahidi huru hatakiwi kuwa mtu mwenye uhusiano na mtuhumiwa kwa namna yoyote, lakini alikana kuwa shahidi huru waliyemtoa kwenye grosari waliyokamatwa washtakiwa alipishana kauli na Adamoo.

Anadai hakuwahi kusikia kutoka kwa Afande Kingai, Mahita wala Jumanne kuitwa viongozi wa Serikali ya Mtaa katika tukio la kuwakamata watuhumiwa Rau Madukani.

Shahidi anadai hakumwambia Jaji kwanini hakukabidhi vielelezo kwa Afande Nuru saa 12 kasoro alfajiri Agosti 7, mwaka 2020, baada ya kufika na watuhumiwa Kituo Kikuu cha Polisi Dar es Salaam wakitokea Moshi.

"Simu za mshtakiwa Halfani Bwire zilichukuliwa na ACP Ramadhan Kingai, nilipewa nishike lakini si kwa makabidhiano.

"Nilizishika kutoka Polisi Chang'ombe hadi Kituo Kikuu cha Polisi, nikiwa njiani sikuwa na mashahidi huru wala mshtakiwa Bwire," anadai shahidi wakati akijibu maswali.

Shahidi anadai Agosti 4, mwaka 2020, ndipo alipisikia kulikuwa na njama za kumdhuru Lengai Ole Sabaya, lakini kabla ya hapo hajawahi kusikia.

Pia anadai kama mpelelezi hajawahi kusikia njama za kuchoma kituo cha mafuta Arusha.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Bwire, Kasekwa na Ling'wenya ambao wanashtakiwa kwa kula njama, kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei mosi na Agosti 5, mwaka 2020.

## Wanafamilia mbaroni kwa tuhuma za mauaji

**Na Rose Jacob,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mwanza, linawashikilia watu watano wakiwamo mke na mume kwa madai ya kuhusika na mauaji ya wanandugu watatu waliokutwa wameuawa na miili yao kutupwa mto Jellys eneo la Buzuruga wilayani Ilemela mkoani humo.

Aidha, limeeleza chanzo cha mauaji hayo ya kikatili ni kudaiana fedha katika biashara ya maharage waliyokuwa wakifanya marehemu na waliopanga mauaji hayo. Polisi wamesema mauaji hayo yalifanywa na watu wa familia moja dhidi ya nyingine ambao ni marehemu na kwamba chanzo chake ni kudaiwa fedha za biashara ya maharage.

Kwa mujibu wa Kamanda Ramadhani Ng'anzi, mauaji hayo yalipangwa na Deoglas Vicent (26) na mke wake Hajira Thomas (24), ambao wanadaiwa kushirikiana na watu wegine kupanga njama za mauaji hayo.

Watuhumiwa wengine ni Thomas Jilala (26) msukuma mkokoteni, Hajira Thomas (23), fundi cherehani, Deoglas Vicent (31) muuza duka la vifaa vya umeme, Emmanuel Mathew (19), wakazi wa Buhongwa na Emmanuel Charles (36) ambaye ni dereva wa mitambo katika mgodi wa Mwadui na mkazi wa Mecco Kusini.

Waliouawa ni Mary Charles (46) ambaye alikuwa mfanyabiashara na mama wa familia hiyo na binti yake, Jenifa Fredy (22) na Monica Jonas (19), mfanyakazi wa ndani wote wakazi wa Mecco.

Mauaji hayo yalitokea Januari 18, mwaka huu, majira ya usiku katika Mtaa wa Mecco Kusini wilayani Ilemela.

"Chanzo cha mauaji hayo ni mgogoro wa kibiashara kati ya Mary ambaye alikuwa akileta biashara zake kutoka Kigoma, kuwapatia baadhi ya watuhumiwa ambao walishindwa kumlipa fedha zake kisha kupanga njama ya mauaji hayo," alibainisha Ng'anzi.

"Baada ya kufanya mahojiano na watuhumiwa hao walikiri kutenda mauaji hayo kwa kuwakata kata mapanga kichwani na shingoni marehemu Mary na familia yake, kisha kupora simu tatu aina ya Tecno kisha kuzifukia shimoni na kuondoka na godoro moja, TV mbili aina ya Singsung zote nchi 18, redio 2, jiko moja la gesi na friji moja aina ya Kyoto," alisema Ng'anzi.

Aidha, Ng'anzi alisema baada ya kupata taarifa za tukio hilo Januari 19, mwaka huu, polisi walianza uchunguzi hadi kufikia Januari 23, waliwakamata watuhumiwa hao pamoja na vitu mbalimbali vya marehemu ambavyo vilinatumiwa na ndugu wa Mary.

Alisema polisi inaendelea kuwatafuta watuhumiwa ambao hawajakamatwa.


A PRODUCT OF The Coca-Cola Company

KILIMANJARO DRINKING WATER

TAARIFA KWA UMMA

**BONITE BOTTLERS LTD** inapenda kuufahamisha umma juu ya kusitisha matumizi ya **plastiki laini (seal)** katika vifuniko vya chupa za **Maji ya Kilimanjaro** kutokana na agizo la serikali juu ya matumizi ya plastiki hizi kulinda mazingira.




@kilimanjaro_drinking_water kilimanjarodrinkingwater kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422

BancABC part of atlasmara

## AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 31 Dec 21 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 30 Sep 21 |
|---|---|---|---|
| **A** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 3,452 | 6,574 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 12,706 | 14,624 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 43,681 | 43,837 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 9,118 | 4,576 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 105,436 | 104,375 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 129,669 | 127,516 |
| | | - | - |
| 12 | Mali Nyingine | 29,077 | 30,769 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,000 | 1,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 2,937 | 3,093 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **337,076** | **336,365** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 92,521 | 91,519 |
| 18 | Amana za Wateja | 134,465 | 129,815 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,576 | 2,052 |
| 28 | Madeni | 77,248 | 77,093 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **305,810** | **300,479** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **31,266** | **35,885** |
| **C** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 122,954 | 122,954 |
| 32 | Hifadhi isiyosambazwa | 1,716 | 1,716 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (87,099) | (86,263) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (7,294) - | 3,511 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 989 | 989 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **31,266** | **35,885** |
| | | (0) | - |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 674 | 3,680 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 17,252 | 18,575 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 11,862 | 13,011 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 9.28% | 10.67% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 12.19% | 13.22% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 62.35% | 63.49% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 38.47% | 37.91% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 47.81% | 48.03% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 2.55% | 4.12% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 0.21% | 2.45% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 31 Dec 21 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita 31 Dec 20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31 Dec 21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31 Dec 20 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 10,554 | 10,657 | 40,865 | 42,736 |
| 2 | Gharama za Riba | (5,427) | (5,110) | (20,403) | (19,652) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **5,127** | **5,547** | **20,462** | **23,084** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 120 | 716 | 439 | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | - | (200) | - | (1,278) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **890** | **1,125** | **4,344** | **5,991** |
| 6.1 | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 200 | 274 | 898 | 1,326 |
| 6.2 | 6.2 Ada na Kamisheni | 288 | 224 | 971 | 4,665 |
| | 6.3 Gawio | - | - | 35 | - |
| 6.3 | 6.4 Mapato Mengine | 402 | 626 | 2,440 | - |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(9,764)** | **(8,807)** | **(32,260)** | **(31,803)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,720) | (2,769) | (10,328) | (10,473) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | (1,077) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (7,044) | (6,038) | (21,932) | (20,253) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(3,626)** | **(1,619)** | **(7,015)** | **(4,006)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (157) | - | - | - |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(3,783)** | **(1,652)** | **(7,294)** | **(4,152)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(3,783)** | **(1,652)** | **(7,294)** | **(4,152)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 167 | 163 | 167 | 163 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (1.54) | (0.67) | (0.74) | (0) |
| 15 | Mapato yaliyopatikana kwa Kushiriki | - | - | - | - |
| 16 | Idadi ya Matawi | 6 | 6 | 6 | 6 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | 0 | - | 0 | - |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -1.12% | -0.50% | -2.17% | -1.20% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -11.27% | -4.01% | -21.72% | -10.17% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 162.27% | 132.00% | 130.23% | -109.38% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 0.72% | 0.78% | 2.85% | 2.11% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 31 Dec 21 | Robo Mwaka iliyopita 30 Sep 21 |
|---|---|---|---|
| **I** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (3,626) | (1,535) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 787 | 776 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (2,990) | (2,080) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 5,651 | 8,760 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 156 | (1,011) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (476) | 588 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 1,692 | 689 |
| | - Kodi Iliyolipwa | (157) | (10) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **1,037** | **6,177** |
| **II** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (630) | (2,716) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(630)** | **(2,716)** |
| **III** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 156 | 237 |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **156** | **237** |
| | | - | - |
| **IV** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 563 | 3,697 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 130,149 | 126,452 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **130,712** | **130,149** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 MACHI 2020

(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(80,525)** | **130** | **0** | **1,065** | **43,624** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (3,252) | - | - | - | (3,252) |
| Hisa za upendeleo | - | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (2,144) | 2,144 | - | - | 0 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(85,921)** | **2,274** | **0** | **1,065** | **40,372** |
| | - | - | - | - | - | - | - |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **116,014** | **-** | **(72,910)** | **0.22** | **1,284** | **1,065** | **45,453** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (8,769) | - | - | - | (8,769) |
| Hisa za upendeleo | 6,940 | - | - | - | - | - | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (130) | 130 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 1,284 | - | (1,284) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **122,954** | **-** | **(80,525)** | **130** | **0** | **1,065** | **43,624** |

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Ofisa Mtendaji Mkuu | I. John | | 25th January 2022 |
| Mkuu wa Fedha | H. Kharbush | | 25th January 2022 |
| Mkaguzi Mkuu wa Ndani | J. Kilato | | 25th January 2022 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 Mkurugenzi | P. Ishengoma | | 25th January 2022 |
| 2 Mkurugenzi | Mr.R. Dave | | 25th January 2022 |

216665302

HABARI KITAIFA

# Nipashe yamwezesha Bahati kuanza kidato cha kwanza

**Na Christina Mwakangale**

ASASI ya Mama Africa Foundation (SAMAFO) na wadau wa elimu, wamelishukuru gazeti la Nipashe kwa kutoa taarifa kuhusu mwanafunzi Bahati Ngolikwa (14), ambaye amepata msaada na kuchangiwa fedha ili kujiunga na kidato cha kwanza.

Bahati ambaye alihitimu darasa la saba Shule ya Msingi Juhudi, iliyoko Halmashauri ya Mbeya Vijijini, mwaka jana, alichaguliwa kujiunga na shule ya sekondari vipaji ya wasichana Galijembe, mwaka huu, ingawa alikumbwa na vikwazo ili kuhudhuria masomo.

Wiki iliyopita Nipashe ilichapisha taarifa gazetini kuhusu Bahati, akiomba msaada kielimu kutoka kwa wadau, baada ya mama na baba yake kudaiwa kumtelekeza na kuishi na bibi na babu yake, ambao hawana uwezo kifedha.

Mkurugenzi Mtendaji wa Sauti ya SAMAFO, Tabitha Bugali, akizungumza na gazeti hili jana, alisema anatoa shukrani baada ya kufanikiwa kumfikisha shuleni binti huyo kutokana na kupatikana fedha za awali kutoka kwa wadau.

Alisema kati ya fedha zinazohitajika takribani Sh. 980,000 zimepatikana Sh. 436,000 ambazo zimemfanya binti huyo kuripoti shuleni ili kuanzia masomo kwa muhula wa kwanza.

"Mungu awabariki gazeti la Nipashe na wadau wote ambao wengi hawakutaka kutaja majina yao. Bahati ameripoti shuleni mwishoni mwa wiki," alisema Tabitha.

Aidha, alisema ambao wataendelea kuguswa watumie akaunti ya shule kumchangia binti huyo, ambayo ni Galijembe Girls Secondary School - NMB A/C Namba 61010036195.

Akizungumza Bahati alisema, ana ndoto ya kuwa daktari, na kwamba anaishi kitongoji cha Iwindi, Kata ya Iwindi, pamoja na bibi na babu yake na wadogo zake wawili ambao hawamjui baba huku mama yao mzazi akiwatelekeza miaka mingi.

"Nilijisikia furaha kubwa nilipochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka wa masomo 2022, changamoto ilikuwa malipo ya ada nilikochaguliwa, lakini sasa nipo shuleni ninashukuru," alisema Bahati.

# Benki CRDB yapunguzia riba wakulima, wafanyabiashara

**Na Maulid Mmbaga**

BENKI ya CRDB imepunguza riba katika mikopo ya vikundi vya wakulima kutoka asilimia 20 hadi tisa na kwa wafanyabiashara kutoka asilimia 16 hadi 13, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la serikali katika kuchochea ukuaji wa uchumi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Abdulmajid Nsekela, punguzo hilo limekuja kufutaia agizo la Rais Samia Suluhu Hassan kwa benki kupunguza riba ili kuchochea uchumi.

Alisema punguzo hilo linatoa ahueni kwa wateja wa benki hiyo kulipa mikopo yao kwa riba nafuu, viwango vya chini vya marejesho ya awali, pamoja na kupata wigo mpana wa kukopa.

"Kwa ushirikiano mkubwa na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) ambaye ndiye msimamizi wa sekta ya benki nchini, mwishoni mwa mwaka jana tuliweza kukaa chini na kuanza kupitia upya riba za mikopo mbalimbali inayotolewa na benki yetu na hivyo ninajivunia kuona leo hii tumekuja na suluhisho la kilio cha muda mrefu cha wateja wetu," alisema Nsekela.

Kadhalika, alisema punguzo la asilimia tisa kwa mikopo ya kilimo ilitolewa ili kusaidia kuimarisha sekta ya kilimo ambayo huchangia zaidi ya asilimia 26 ya Pato la Taifa na kutoa ajira kwa asilimia 75 ya Watanzania.

Sababu ya kutoa punguzo hilo alisema kuwa ni kuchochea kasi ya mapinduzi katika sekta ya kilimo nchini kwa kuwawezesha wakulima wadogo na wakati kufanya kilimo cha kisasa kupitia mikopo nafuu ya pembejeo na zana za kilimo.

Aidha, alisema kuwa benki hiyo imetoa asilimia 40 ya mikopo yote ya kilimo nchini, huku akibainisha kwamba katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, walitoa mikopo ya zaidi ya Sh. trilioni 1.6 kwa wadau wote katika mnyororo wa thamani katika kilimo, huku akitolea maelezo na kwa upande wa wafanyabiashara pia.

"Wafanyakazi ni kundi muhimu kwa benki yetu ndio maana tumekuwa tukiboresha kwenye riba ya mikopo ya kundi hili kila mwaka ili kuwasaidia kufikia malengo waliyojiwekea jambo ambalo litaongeza ufanisi katika maeneo yao ya kazi, pia msikope bila kuwa na malengo.

"Hii ni mara ya tatu ndani ya miaka mitano iliyopita kwa benki yetu kupunguza riba ya mikopo ya wafanyakazi, matarajio yetu ni kuwa wafanyakazi watachangamkia fursa hii ili kuboresha maisha yao na hilo ndio haswa lengo la Benki ya CRDB," alisema Nsekela.

Kwa miezi kadhaa sasa serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BOT) imekuwa ikitoa wito kwa taasisi za fedha kupunguza riba kwa wateja ili kuimarisha uchumi.

Kufanikisha hilo Benki Kuu imechukua hatua mbalimbali za kisera ikiwamo kupunguza kiwango cha sehemu ya amana za benki kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu, pamoja na kuanzisha mfuko maalum wenye thamani ya shilingi trilioni moja ambao utatumika kukopesha benki na taasisi za fedha kwa riba ya nafuu, ili ziweze kukopesha sekta binafsi.


BancABC part of atlasmara

AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED

MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| | PRICING (TZS) | PRICING (US $ / EUR) | PRICING (GBP) |
|---|---|---|---|
| **PERSONAL BANKING** | | | |
| **SAVINGS ACCOUNT** | | | |
| **IZZE** | | | |
| Account Opening Fee | Free | NA | NA |
| Opening balance | Free | NA | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NA | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 10,000.00 | NA | NA |
| Monthly Service Fee | Free | NA | NA |
| | | | |
| **FAHARI** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Monthly Service Fee | TZS 1,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| | | | |
| **MWANGAZA JUNIOR ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 20,000.00 | $ 500.00 | £ 500.00 |
| Monthly Service Fee (1 free w/drawal per quarter) | Free | Free | Free |
| Extra fee for more than 1 w/drawal per quarter | TZS 5,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| | | | |
| **WEKEZA SAVINGS ACCOUNT (BALANCE BUILD UP)** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | Free | Free | N/A |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 100,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | N/A |
| | | | |
| **CURRENT ACCOUNT** | | | |
| **AMANA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | N/A | N/A |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | N/A | N/A | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| | | | |
| **MARIDHAWA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 25,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 6,000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| | | | |
| **PREMIUM** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 35,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| | | | |
| **SME BANKING** | | | |
| **AMANA BIZ ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 50,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| | | | |
| **SME TIERED CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | TZS 1,000,000.00 | $ 1,000.00 | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 5,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 15.00 | NA |
| | | | |
| **JAMII CURRENT ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | Free | Free | Free |
| Minimum Operating Balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 50,000.00 | £ 50,000.00 |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | Free |
| | | | |
| **CORPORATE BANKING** | | | |
| **CORPORATE CURRENT ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | £ 250.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NA | NA | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| | | | |
| **CORPORATE CALL ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 1.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| | | | |
| **CORPORATE TIERED INTEREST ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | NA |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | NA |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NA |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000,000.00 | $ 100,000.00 | NA |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | NA |
| | | | |
| **GENERAL CHARGES** | | | |
| Bankers Cheque | TZS 50,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| | | | |
| DISHONORED/UNPAID CHEQUE | | | |
| Fund related | TZS 120,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| Technical | TZS 30,000.00 | $ 50.00 | N/A |
| | | | |
| **Cheque book Processing Fee:** | | | |
| 25 leaves | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 50 leaves | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 20.00 |
| 100 leaves | TZS 50,000.00 | $ 35.00 | £ 35.00 |
| Uncollected cheque book after 3 months | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 3rd party encashment (with 3rd party indemnity) | TZS 25,000.00 | 1% Per Cheque + $20 | 1% Per Cheque +$20 |
| Stop Payment Charges | TZS 30,000.00 | $ 25.00 | £ 25.00 |
| | | | |
| **TRANSACTIONAL SERVICE FEES** | | | |
| **With banks via Standing Orders** | | | |
| Standing Order - internal same customer ( set up fee - once off) | Free | Free | Free |
| Standing Order - internal other customers ( per transaction) | Free | Free | Free |
| Standing Order - Other local bank | TZS 20,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Amendment | Free | Free | Free |
| | | | |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS:** | | | |
| Cash Deposit at Branch | Free | Free | Free |
| Cash Deposit at Branch coins above 100,000 | 5% Min 10,000 | NA | NA |
| Cash Deposit at Branch small denominations less than 50USD (USD 1,2,5,10,20) equal and above USD 500 | NA | 3% of FCY currency value | 3% of FCY currency value |
| With Account Transfers (Internal) | Free | Free | Free |
| Cheque deposit | Free | Free | Free |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) up to 2m | TZS 3,500.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) btn 2m to 20m | TZS 4,000.00 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) above 20m | 0.15% Max 50,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal SME ( over the counter) | 0.15% Min 3,000 Max 20,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Cash withdrawal Corporate Banking | 0.15% Min 3,000 Max 100,000 | 1% Min 5 | 1% min 5 |
| Deposit charges - Financial Institution. | Free | Free | Free |
| Deposit charges - Financial Institution - small denominations | Free | 3% On small denominations above $500 | 3% On small denominations above $500 |
| | | | |
| Account Closure | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account Reactivation | NIL | NIL | NIL |
| Dormant Account monthly fee | NIL | NIL | NIL |
| Premature/cancellation fixed deposit fee | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited |
| Monthly statements | Free | Free | Free |
| Interim Statements (per page) | TZS 2,000.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| Search fee documents (after 3 months) | TZS 80,000.00 | $ 40.00 | £ 40.00 |
| Audit confirmation | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Balance Certificate | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Reference Letter | TZS 50,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Inter Account Transfers | Free | Free | Free |
| T T Outward local - TISS | TZS 11,800.00 | $ 10.00 | N/A |
| T T Outward local - EFT | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| T T Inward local TISS | Free | Free | N/A |
| Salary processing (per entry) | TZS 1,500.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| International Outward T T | N/A | $50 + Other overseas bank chrges | $50 + Other overseas bank chrges |
| International Inward T T | N/A | Free | Free |
| Travellers Chq. Deposit | N/A | N/A | N/A |
| Foreign BankDrafts | N/A | $ 50.00 | £ 30.00 |
| Outward Cheque for Collection | N/A | N/A | N/A |
| Outward Bills for collection | N/A | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) |
| Inward Bills for Collection | N/A | 0.25% MIN 50 | 0.25% MIN 50 |
| Advising fee (Inward Bill & LCs ) | N/A | $ 200.00 | £ 200.00 |
| Travellers Chq. (Issue) | N/A | N/A | N/A |
| Letters of Credit | N/A | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) |
| Bank Guarantees | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% Per Qtr Min $ 200 |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wananchi waelimishwe mabadiliko ya tabianchi

**WATAALAMU** wa mazingira wanaeleza kuwa kina cha Ziwa Tanganyika kimeongezeka kwa asilimia mbili kiasi cha kuathiri shughuli za kiuchumi na maisha ya watu kwa ujumla.

Tayari maeneo ya huduma za jamii kama shule, vyuo, zahanati na vituo vya afya vimezingirwa na maji kiasi cha kushindwa kutumika, huku makazi ya watu yakiharibiwa vibaya.

Ziwa hilo ambalo ni la pili kwa ukubwa duniani likiwa mpakani mwa Tanzania kwa asilimia 46, huku sehemu ikiwa Zambia, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo asilimia 40, kote shughuli za uvuvi wa mazao ya samaki yanafanyika ambao umekuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Kutokana na kuongezeka kwa maji mwalo wa Kibiziri, Kigoma Ujiji umefunikwa kiasi kwamba wafanyabiashara wa dagaa na samaki hawawezi kuendelea na shughuli zao, wametawanywa kwenye maeneo mengine ili waendelee kujitafutia mahitaji.

Wengi maisha yao yamebadilika kwa kuwa wamelazimika kuanza kutumia mitaji yao, kujifunza shughuli nyingine kama kuuza maandazi na kushona mashuka, baadhi wanasema wameshindwa kusomesha watoto wao kwa kuwa fedha wanayopata inatosheleza mlo mmoja kwa siku na siyo kununua madaftari, sare za shule, viatu na mabegi.

Wanawake wajasiriamali wameeleza maisha yao kuwa kabla ya kuongezeka kwa maji waliuza dagaa au samaki kwa Sh. 40,000 hadi 60,000 na kupata kati ya Sh. 5,000 hadi 20,000 kwa siku ambayo iliwasaidia kuboresha maisha yao.

Kwa sasa wapo wanaoingiza Sh.2000 kwa siku ambayo hutumiwa na familia kupata mlo mmoja ambao huliwa saa 10 jioni, huku wengine hawana uhakika wa kupata hata Sh.100.

Pia kutokana na mabadiliko ya tabianchi, idadi ya samaki imepungua, huku wakilazimika kuwafuata mbali hali inayopandisha bei na wengi kushindwa kuendelea na biashara hiyo kama ajira.

Shughuli za kiuchumi za mkoa wa Kigoma ni uvuvi na kilimo, wengi wakitegemea ziwa hilo kukua kiuchumi hasa kwenye kuuza samaki na dagaa, lakini hali inavyokuwa hivyo ni hasara na wengi wanarudi kwenye umaskini.

Mabadiliko ya tabianchi si tukio la kushtukiza bali hutokea taratibu huku kukiwa na viashiria vingi, ambavyo kwa jamii iliyoelimishwa ni rahisi kutambua na kuchukua hatua.

Tunatambua kuwa mabadiliko hayo ni suala la kidunia, lakini jamii na nchi inaweza kufanya jitihada za kutunza mazingira kiasi cha kurejesha ubora wake, lakini wanaweza kujiandaa mapema kuwa na shughuli mbadala.

Mathalani, taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na watafiti mbalimbali zinaweza kuwafikia wananchi katika ngazi ya chini kabisa, ili wanapofanya maamuzi ya kulima mazao fulani au kuendelea na shughuli fulani wajue mabadiliko yaliyoko.


Kila jamii ina namna ya kutambua viashiria vya hatari kwenye maeneo yao, baadhi wakitumia wazee wa zamani kuwaeleza historia ya eneo na kujua kikitokea kitu fulani ni dalili ya jambo fulani kutokea, ili wajue hatua za kuchukua.

Ni muhimu wananchi wakafundishwa ikiwamo kuwa na shughuli mbadala ili yanapotokea mabadiliko kama haya au majanga mengine waweze kuendelea na maisha, hili ni jukumu la serikali kuhakikisha elimu hiyo inawafikia wananchi.

Tunajua serikali imeridhia mikataba mbalimbali ikiwamo Sendai Frame Work, kwa ajili ya nchi kuwa na mikakati ya kukabili majanga pamoja Malengo Endelevu ya Milenia (SDGs).

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# TARURA mnaongeza machozi zaidi Msumi

Na Mwandishi Wetu

**NI** kama mwezi umetimia sasa tangu kuanza matengenezo ya barabara ya Madale Msumi jijini Dar es Salaam, ikitengenezwa kwa 'kiwango cha vumbi'

Kinaweza kuitwa kiwango cha vumbi kwasababu njia hiyo inamwagwa vifusi vya mawe madogo ambavyo havisambazwi na kushindiliwa kikamilifu.

Kinachotokea baada ya kusambaza vifusi vya kiasi kidogo na kuacha vurumai barabarani ni kuwaachia watumia barabara zawadi ya vumbi muda wote hasa msimu wa kiangazi na matope msimu wa mvua.

Nirejee kwenye barabara ya Madale Msumi wilayani Ubungo, eneo la njipanda ya Mbopo kwenda Msumi Centre, barabara hiyo imekuwa kero kwa wananchi na kuzidi kuwaongezea kilio.

Kipande hicho cha barabara pengine chenye urefu wa kilomita tatu, kimemwagwa kifusi tangu kuanza mwaka huu lakini, hakijasambazwa wala kushindiliwa kikamilifu.

Matokeo yake ni udongo au kifusi kusambaa pembeni ya barabara na kusababisha adha muda wote mvua zinaponyesha.

Wakati huu wa mvua kifusi hicho kinachojaa pembeni ya barabara zisizo na njia za maji kimesababisha malori ya shehena kama saruji, kokoto, mchanga na magari na vifaa vya ujenzi kunaswa na kukwama.

Aidha, imekuwa kero kwa wanafunzi wanaosoma shule za Goba, Msumi, Madale na Makabe kukwama kwenda shule asubuhi kurudi jioni wakilazimika kubadilisha njia na hata kutishiwa maisha kwa sababu ya utelezi barabarani.

Yote hayo, yanatokana na udongo au kifusi kilichorundikwa kugeuka tope na kusababisha magari kutitia yanapojaribu kupishana.

Inakuwa vigumu kuyakwamua kutokana na tope hilo, hivyo kuchelewesha shughuli nyingi za maendeleo hasa kwa wakazi wanaotumia barabara ya njiapanda hiyo ya Mbopo-Msumi.

Matatizo ya usafiri kwa wakazi wa Mbezi Msumi ni mengi kwa vile ni eneo ambalo kwa muda mrefu lilikuwa nyuma na hivi karibuni kinamama wa eneo hilo walimpatia Waziri wa Maji, Jumaa Awesu, dumu la maji machafu wanayotumia kwa vile sehemu hiyo haina majisafi ya bomba wala visima vya DAWASA.

Aidha, pamoja na maji tatizo la barabara ni kubwa na hata pale Wakala wa Barabara za Miji na Vijijini (TARURA) anapojenga barabara za eneo hilo, malalamiko hayaishi.

Hata sasa, wananchi wanaendelea kuilalamikia TARURA kwa kushindwa kushindilia na kuchonga mifereji ya maji kando ya barabara hiyo na kusababisha usumbufu kila wakati.

Wakazi wa Msumi wanaikumbusha mamlaka hiyo ikamilishe kazi ya kutengeneza kipande hicho cha barabara hiyo kwa sababu kumwaga kifusi bila kukisambaza na kukishindilia kikamilifu ni kuharibu fedha za umma na kukera walipakodi.

Uharibifu kwa sababu hakisambazwi na kushindiliwa matokeo yake ni kukiharibu na kuongeza tena hasara kwa walipa kodi. Lakini haiishi hapo, kukwangua barabara na kuzishindilia bila kuweka njia za maji ni sababu inayoongeza barabara kuharibika kila wakati.

Hili nalo TARURA iliangalie ili ituondolee machozi wana Msumi.

Kwa upande mwingine ingependeza kama serikali ingetengeneza barabara za lami nyepesi badala ya kuendelea na ujenzi wa kukwangua na kumwaga kifusi kila mara, hatua inayotumia fedha nyingi lakini bila ufanisi.

Wakazi wa Msumi wanaomba serikali iwafanyie wepesi kwa sababu mvua zikianza kunyesha mfululizo hasa wakati wa masika maisha na usafiri utakuwa mgumu na kukwamisha shughuli zao kutokana na gharama kuongezeka.

Kuchonga barabara kusionekane kama jambo la kusaidia bali la muhimu kwa maendeleo kwa vile bila usafiri na usafirishaji shughuli zote za kiuchumi zinakwama.

TANGAZO

# MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

**Imethibitishwa na ISO 9001: 2015**

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU
## WAJIBU WA KUDAI RISITI ZA EFD KWA WANUNUZI WA BIDHAA AU HUDUMA

**Dar es Salaam, Januari 21, 2022:**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwakumbusha wanunuzi wote wa bidhaa au huduma kuhakikisha wanadai risiti za EFD pale wanapofanya manunuzi ili kutimiza wajibu wao wa kisheria. Aidha, wanunuzi wote wa bidhaa au huduma wanakumbushwa kuhakikisha thamani iliyo kwenye risiti ni sawa na kiasi cha fedha walicholipa au wanachotakiwa kulipa.

**Kifungu cha 36 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438** kinatoa wajibu kwa muuzaji wa bidhaa au huduma kutoa risiti ya EFD pindi anapofanya mauzo na vilevile **Kanuni ya 55(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Kodi ya Mwaka, 2016** inampa wajibu mnunuzi wa bidhaa au huduma kudai risiti pale anapofanya manunuzi na kuionyesha kwa Kamishna au Afisa wa Kodi pindi anapotakiwa kufanya hivyo.

Ni kosa kisheria kwa mnunuzi yeyote kutokudai risiti pindi anaponunua huduma au bidhaa. Kwa mujibu wa **Kifungu cha 86(4) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438**, mnunuzi atakayebainika kutodai risiti atawajibika kulipa faini isiyopungua **TZS 30,000** na isiyozidi **TZS 1,500,000** kama adhabu.

Hivyo wanunuzi wote wa bidhaa au huduma wanakumbushwa kuendelea kudai risiti za EFD na iwapo muuzaji wa huduma hiyo au bidhaa hatampatia risiti, mnunuzi anatakiwa kutoa taarifa katika Ofisi za TRA zilizopo jirani naye kama inavyoelekezwa kupitia **Kanuni ya 55(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Kodi ya Mwaka, 2016** au kupiga simu kupitia namba ya bure ya huduma na elimu kwa mlipakodi ambazo ni **0800 750 075 au 0800 780 078.**

Kuanzia tarehe **01/02/2022** TRA itafanya operesheni maalumu za ukaguzi wa risiti za manunuzi ya bidhaa na huduma katika maeneo mbalimbali nchi nzima ikilenga kuhakikisha kila mnunuzi anatimiza wajibu wake wa kisheria kwa kudai risiti pale anapofanya manunuzi.

***Epuka usumbufu, ukiuza toa risiti na ukinunua dai risti.***

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na;

**A.J Kidata**
**KAMISHNA MKUU**
**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

216662702

RIPOTI MAALUM

# Kina Ziwa Tanganyika kilivyoliza wajasiriamali -2



Baadhi ya wavuvi na wanawake wajasiriamali wa dagaa na samaki wakiwa kwenye mwalo wa Kibiziri, ambao umefunikwa na maji kutokana na kuongezeka kwa kina cha maji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Na Salome Kitomari**

**KATIKA sehemu ya kwanza ya ripoti maalum hii, wanawake wajasiriamali wa samaki na dagaa waliokuwa kwenye Mwalo wa Kibirizi, mkoani Kigoma, wakieleza hali ngumu ya uchumi baada ya kuongezeka kwa kina cha maji cha Ziwa Tanganyika, katika sehemu hii ya mwisho watafiti, serikali inafafanua hatua zilizochukuliwa. Endelea...**

Anasema biashara wanazofanya kwa sasa zinawawezesha kupata faida ya Sh. 3,000 au 4,000 ambayo hawawezi kuigawa kwa ajili ya mahitaji ya familia na kusomesha watoto na ndiyo maana hadi sasa mwanawe hajaenda shule anasubiri kupata sare za shule. Naye Hadija Sabuni, mkazi wa Karago, anasema alihamia eneo la biashara na familia yake lakini baada ya kina cha maji kuongezeka ilibidi ahame na sasa anafanyabiashara ndogondogo.

"Maji yameingia kwenye Mwalo huwezi tena kuuza, wateja wameondoka hatuna mahali pazuri pa kununua mzigo, tumeanguka kiuchumi sana kwa sasa tumeishia kupata fedha ndogo ndogo, kazi kuuza samaki na dagaa niliitegemea kusomesha watoto," anasema.

Anasema kuna nyumba zimeanguka na kuzolewa na maji, lakini wanaamini mipango ya Mungu kwa kuwa ndiye mpangaji, na sasa wamebaki kuomba msaada wa ndugu walioko mjini ili maisha yaweze kuendelea.

Aisha Zuberi, Mkazi wa Livingi Stone anayefanyabiashara ya masende, anasema amegeukia biashara ya maandazi ambayo nayo ni shida sana kupata wateja.

"Boti zinakuja bure wanauza kwa shida, anasema mtaji wake ulikuwa 200,000 na aliweza kuuza na kupata kati ya Sh. 15,000 hadi 20,000 na kupata watoto, na sasa nimeingia kwenye kufuma mashuka na kuuza maandazi ili niendeshe familia," anasema.

Aidha, anaiomba serikali kuwasaidia kwa kuwajengea eneo jingine la biashara ili maisha yaweze kuendelea.

Zawadi Mfaume, anasema alianza kuuchuza samaki wabichi tangu mwaka 1992, amesomesha mwanawe hadi kidato cha nne na kujenga nyumba kwa kazi hiyo, lakini changamoto kubwa ni kuongezeka kina cha maji ambako kumewafanya waondoke kwenye eneo hilo.

"Baada ya kujaa maji eneo lile tulihamishiwa eneo hilo, tumechangamana wa mboga, samaki wa wabichi na wakavu na inawapunguzia watoto. Naendelea na hii kazi ili watoto wangu waende kusoma, nimesomesha watoto na kujenga nyumba.

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Samaki na Dagaa Kibirizi, Machumu Yenda, anasema changamoto kubwa ni upatikanaji wa uhakika wa samaki, kwa kuwa kutokana na mabadiliko ya tabianchi hawapatikani kwa wakati.

"Hali ya sasa na zamani ni tofauti, mazao tunayoona sasa ni madogo mno ukianzia mwambao wa Kagunga hadi Kibirizi, lakini sasa wanavua kwenye kina kirefu na wanapatikana kwa tabu sana," anasema.

Anasema asilimia kubwa ya wakazi wa Kigoma wanategemea Ziwa Tanganyika na kwamba hali imezidi kuwa ngumu, mzunguko wa zamani sio wa sasa, wanaiomba serikali kusaidia wapate zana bora ili wavuvi wakavue kirahisi. Anasema kipindi cha nyuma soko hilo lilikuwa na uwezo wa kupokea tani tatu, lakini kwa sasa inapatikana nusu tani, hali ambayo imeshusha pato la mtu mmoja mmoja, mkoa na taifa kwa ujumla.

Suzanna Ezekiel, mmiliki wa zana za uvuvi na mchakataji katika Mwalo wa Kibirizi, anasema mabadiliko hayo yamewaathiri kwenye mnyororo wa thamani wa mazao yao, huku akisema kipindi cha masika na vuli hawana mahali pa kuanikia samaki kwa kuwa eneo limejaa maji.

Naye mvuvi George Kalea anasema, kutokana na kuongezeka kwa kina hicho wanalazimika kutumia vifaa vya kisasa ili kupata mazao lakini imeshindikana na matokeo yake kufanyakazi kwa mazingira magumu.

**UTAFITI**

Naye Mtafiti wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), Prisca Mziray, anasema kasi ya upepo ambao husaidia maji kuchanganyika imepungua huku joto likiongezeka na kwamba kwenye maji kuna tabaka la juu ambao ni joto, la kati ni joto kiasi na la chini baridi na ili yachanganyike inabidi joto la kati ya tabaka moja na jingine isiwe kubwa sana.

"Sasa kutokana na joto kuongezeka sana linafanya tabaka la juu kuwa na joto sana kwa hiyo haya maji kuchanganyikana inakuwa vigumu, uwezo wa maji ya chini kuja juu inakuwa ngumu na ziwa linazidi kuwa na virutubisho vichache kwa ajili ya mazao ya uvuvi," anasema.

Kwa mujibu wa mtafiti huyo, kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu kama kilimo kandokando mwa Ziwa Tanganyika kumesababisha udongo kuingia ziwani ambao huharibu mazalia ya samaki kwenye miamba pamoja na maji ya viwandani ambaya huingia bila kutibiwa.

**OFISA UVUVI**

Ofisa Uvuvi Mkoa wa Kigoma, Ritha Mlingi, anasema hali ya uvuvi sio ya kuridhisha kwa kuwa mazao yake yamepungua na kinacholetwa kwenye mwalo kimepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

"Zamani mvuvi alikuwa akienda anarudi na hadi boxi tano hadi 20 kwa sasa wanakwenda zaidi ya mmoja anarudi na dagaa nusu ndoo, ni dalili kuwa hali ya uvuvi kwenye ziwa letu sio nzuri, pamoja na kiwango, lakini kuna ukubwa wa samaki mfano mgebuka ulikuwa unapatikana mkubwa ila sasa kwenye mialo rasmi na isiyo rasmi ni midogo sana," anasema.

Aidha, anasema kuna aina ya samaki wamepungua na wengine wametoweka kabisa hali inayoonyesha kuwa hali sio nzuri na kuna hatua zinapaswa kuchukuliwa.

Kwa mujibu wa Mlingi, anasema utafiti utafanyika kujua kiwango cha samaki, na kwamba mabadiliko ya tabia nchi yamechangia kupungua kwa samaki, kwa kuwa ni viumbe ambao huathiriwa kwa haraka kukiwa na mabadiliko.

Anasema jingine ni kuongezeka kwa nguvu inayotumika kwenye uvuvi na kwamba zamani walikuwa wengi kwa kuwa walikuwa wachache, ila sasa wengi wameingia kama sehemu ya ajira na kusababisha kuongezeka kwa eneo la kuvua na uharibifu.

Anasema kwa mujibu wa sheria mtu anaruhusiwa kuvua umbali wa kilomita moja kuendelea kutoka kwenye fukwe, na atakayekutwa anavua chini ya hapo ni uvuvi haramu.

**HATUA ZILIZOCHUKULIWA**

Waliwahamisha wanawake wanaofanya ujasiriamali wa kuuza dagaa wakawapeleka kwenye masoko ya karibu na mialo na waliokuwa na maeneo ya kukaushia yaliyofunikwa na maji waliruhusiwa kujenga maeneo mapya.

"Tulijaribu kujaza maji kwenye mwalo wa Kizuiri ili yasiendelee kuingia na walihamishiwa eneo la jirani na kuna jitihada zinaendelea kuangalia nini kifanyike ili waendelee kufanya biashara zao vizuri zaidi," anasema.

**ZIWA TANGANYIKA**

Kwa mujibu wa mtandao wa Wikipedia, Ziwa Tanganyika ni moja ya maziwa makubwa Afrika ya Kati ni la pili kwa ukubwa duniani kwa wingi wa maji limeenea mpakani mwa Tanzania ikiwa ni asilimia 46, likipakana na nchi za Kongo asilimia 40, Burundi na Zambia. Lina kina cha mita 1,470 na kilomita 600.

Ndani ya ziwa hilo sehemu ya Tanzania kuna Kisiwa cha Kupita, Kongo kuna visiwa vya Kavala, Mamba –Kayenda, Milima na Kibishie, huku Zambia kukiwa na Mutonowe na Kumbula.

**WAZIRI**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, anasema mabadiliko ya tabianchi yamesababisha kuongezeka kwa kina cha maji Ziwa Tanganyika kwa mita mbili jambo ambalo ni hatari, na kwamba kwa sasa wanaendelea na utafiti huku wakihamasisha wananchi kupanda miti.

**Ripoti hii imefadhiliwa na Chama cha Wachapishaji wa Habari Duniani (WAN-IFRA) kupitia Social Reporting Initiative (SIRI).**

# NEMC yataka tathmini athari za mazingira kwa miradi yote

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

SERIKALI imeagiza kufanyika tathmini ya athari za mazingira kabla ya kuanza mradi wowote wa uchimbaji madini na kuweka mpango wa utunzaji wa mazingira mgodi unapofikia mwisho.

Agizo hilo lilitolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, alipofanya ziara kwenye mradi wa mgodi tarajiwa wa Nyanzaga ulioko Kata ya Igalula Wilaya ya Sengerema Mkoa wa Mwanza.

Mgodi huo unaomilikiwa na Kampuni ya SOTTA Mining Corporation.

"Mgodi unapoanzishwa ni lazima ufanyiwe tathmini ya athari za mazingira na mpango mkakati wa utunzaji wa mazingira kabla ya kuanzishwa, unapochimbwa na hatimaye unapofunga ili kulinda mazingira yetu," alisema Dk. Gwamaka.

Aidha, alisema migodi iliyoanzishwa kabla ya Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 inachangamoto nyingi ikiwa ni pamoja na migogoro ya kimazingira kati yake na jamii, pamoja na serikali kuingia gharama kubwa ya kurekebisha mazingira yaliyoharibika.

"Hasara nyingine ya kutokuweka mpango mkakati wa namna ya ufungaji wa migodi pindi unapofungwa ni pamoja na kuacha mazingira katika hatari kwa afya ya jamii na viumbe wengine hai," alisema Dk. Gwamaka.

Alisema ni mkakati wa Baraza kuhakikisha historia mbaya ya utunzaji wa mazingira kwa migodi iliyoanzishwa kabla ya Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 hayatajitokeza tena kwenye migodi itakayoanza kuchimbwa kwenye awamu ya sita.

Naye Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria kutoka NEMC, Mhandisi Redempta Samwel, alipongeza hatua zinazochukuliwa na mradi wa uchimbaji wa madini ya dhahabu wa Nyanzaga katika kuhakikisha mazingira yanatunzwa kuanzia hatua ya awali kabla ya shughuli za uchimbaji kuanza.

Mhandisi Redempta aliongeza kuwa Baraza lina wajibu na mamlaka ya kisheria ya kufuatilia utekelezaji wa mpango mkakati ili kuepusha athari za kimazingira zinazoweza kujitokeza.

Wakati huo huo, Meneja wa NEMC Kanda ya Ziwa Victoria, Jerome Kayombo, alisema mgodi tarajiwa wa Nyanzaga utakuwa ni wa mfano kwa migodi mingine kwasababu umeanza ushirikiano na wataalamu wa mazingira kuanzia hatua za mwanzo kabisa hali ambayo itasaidia kuweka mipango mikakati ya kuzuia uharibifu wa mazingira.

"Sisi baraza tunahakikisha anayeanzisha mgodi amefanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) pamoja na kuweka mpango mkakati wa utunzaji wa mazingira," alisema Kayombo.

Nao uongozi wa mgodi tarajiwa ulipongeza NEMC kuwa taasisi ya kwanza kufika mgodini hapo baada ya kupata cheti cha mazingira na wameahidi kushirikiana nao bega kwa bega kuhakikisha mazingira yanalindwa kwa ajili ya maendeleo endelevu.



Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashantu Kijaji (wapili kushoto), akimsikiliza mmiliki wa kiwanda cha kutengeneza juisi ya embe cha Jambo, Salum Hamis (watatu kushoto), alipofanya ziara ya kuona shughuli za uzalishaji wa bidhaa mbalimbali kiwandani hapo jana. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema. **PICHA: MARCO MADUHU**

## Asiyejulikana adaiwa kujeruhi kwa gogo kichwani

**Na Said Hamdani,** LINDI

SOPHIA Saidi Ruvu (29), mkazi wa Mtaa wa Mchinga, Kata ya RahaLeo, Manispaa ya Lindi, amenusurika kufa baada ya kushambuliwa kwa kupigwa na gogo kichwani na mtu anayedai kutomfahamu.

Tukio hilo linadaiwa kutokea Januari 21, mwaka huu, saa 5:0 usiku.

Ruvu alisema alipatwa na mkasa huo nyumbani kwake, baada ya kurejea kutoka katika shughuli zake za uuzaji wa samaki wa kukaanga eneo la uwanja wa Fisi.

Alisema alipofika ndani alibadilisha nguo kisha kuchukuwa maji kuelekea bafuni kuoga, ndipo mshambuliaji aliyekuwa amejibanza kuta za ukumbi wa nyumba yao, alimtokea nyuma na kumpiga kichwani na kitu kizito na kuanguka chini, huku akipiga kelele za kuomba msaada wa majirani.

"Nikiwa najitayarisha kwenda kuoga sikuwa nafahamu kama ndani mna mtu mwingine mwenye nia mbaya na mimi, alisema Ruvu.

Ruvu aliyejeruhiwa kichwani upande wa kushoto anasema majirani walipofika walimchukua na kumkimbiza Hospitali ya Mkoa, Sokoine na kupewa huduma za matibabu kwa kushonwa nyuzi nne na kurejea nyumbani kwa mama yake mzazi.

Amesema katika tukio hilo, mshambuliaji huyo ameacha ndani ya nyumba anayoishi Sophia Ruvu gogo la mti aina ya mkoko linalodaiwa kutumiwa kumshambulia na tisheti rangi nyekundu yenye maandishi kifuani Uhlsport.

Mwenyekiti wa mtaa huo, Seif Juma na majirani walithibitisha kushambuliwa kwa Ruvu na kueleza walipata msaada wa usafiri kutoka kwa raia mwema aliyekuwa akipita mtaa huo na gari ambaye alisimama na kumchukua hadi hospitalini.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, ACP Mtatiro Kitinkwi, alipotafutwa kupitia simu zake za mkononi, hakupatikana.

# Madiwani waelekeza kilimo cha kisasa Muleba

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

BAADHI ya madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba mkoani Kagera, wamewataka watendaji kuweka mipango thabiti ambayo itawezesha kufanyika kwa kilimo cha kisasa yakiwamo matumizi ya trekta, ili kuinua mapato ya halmashauri kupitia sekta hiyo.

Wamewataka kufanya hivyo badala ya kutegemea mapato yatokanayo na huduma kwa asilimia kubwa.

Wakizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani cha mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2022/2023 madiwani hao akiwamo Elton Isaya wa Kata ya Kibanga walisema kuwa matumizi ya trekta katika kilimo yatasaidia kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara ikiwamo kahawa, migomba, mahindi na maharage, ambayo ni muhimu katika kuinua uchumi wa wananchi, halmashauri na mkoa kwa ujumla.

"Hata sisi madiwani tunalo jukumu kubwa la kuhamasisha wananchi ili kuhakikisha wanabadilika na kuanza kulima kisasa, lakini hamasa pekee haitatosha kama hakuna mipango thabiti ya kuhakikisha upatikaji wa pembejeo kwa urahisi na wananchi kuwezeshwa kielimu na kupata mikopo yenye masharti nafuu, ili waweze kupata vitendea kazi kama trekta kwa lengo la kupanua kilimo," alisema Isaya.

Naye Mkuu wa Wilaya hiyo, Toba Nguvila, alisema kuwa ili waweze kupata mafanikio makubwa katika kilimo, madiwani wanapaswa kuongeza hamasa kwa wananchi kupitia kata zao ili waone umuhimu wa kilimo na faida zake badala ya kuwaacha hasa vijana wakakimbilia mijini kuendesha bodaboda.

"Niwaombe madiwani mhamasishe kilimo katika kata zenu angalau kila kijana awe na shamba lenye ukubwa wa kuanzia ekari moja, hatuwezi kuwa na vijana wanaowaza kuendesha bodaboda tu au wanaotegemea kutunzwa na wazazi wao wakati wana nguvu za kulima," alisema Nguvila.

Alisema kuwa yapo mazao mengi yanayostawi vizuri katika wilaya hiyo ikiwamo kahawa, mpunga, migomba, mahindi na maharage, mazao ambayo wakizalisha ipasavyo wakauza hawawezi tena kuwaza kwenda kuendesha bodaboda.

Kikao hicho kimepitisha mpango na bajeti ya zaidi ya shilingi bilioni 74.4 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Akiwasilisha bajeti hiyo, Ofisa Mipango wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Evath Kagaruki, alisema kuwa zaidi ya shilingi bilioni 5.6 ni mapato ya ndani, zaidi ya shilingi bilioni 1.3 ni ruzuku (Other Charges), zaidi ya shilingi bilioni 48.4 ni ruzuku ya mishahara na zaidi ya shilingi bilioni 19 ni ruzuku ya miradi.

# Walengwa TASAF waeleza walivyoboresha makazi yao

**N Elizabeth Zaya,** HANDENI

WALENGWA wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wameelezea namna walivyotumia pesa wanazopatiwa kutoka katika mpango huo kuboresha makazi yao.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti walipotembelewa na maofisa wa TASAF kutoka makao makuu, walengwa hao walisema kabla ya kuingizwa kwenye mpango huo, walikuwa wakiishi katika nyumba za tope ambazo wamezijenga na miti, lakini kwa sasa wamejenga nyumba za kisasa.

Walisema pamoja na kutumia pesa wanayopatiwa na TASAF katika kununulia mahitaji ya muhimu ya watoto wao wanaosoma, kutumia kwenye chakula na matibabu, lakini walijifunza kuweka akiba kidogo kidogo na kuanzisha miradi midogo ya kujiongezea kipato ambayo iliwasaidia kupata pesa ya ziada ya kuboreshea makazi yao.

"Tunaishukuru sana TASAF kwa sababu wakati wanaanza kutupatia pesa kutusaidia, walitufundisha pia na namna ya kuwa na nidhamu ya kuweka akiba ili itusaidie kuanzisha miradi ya kujiongezea kipato na walisema bila hivyo tutaendelea kuwa tegemezi, kwa sababu pesa tunayopatiwa pekee haitatutosheleza.

"Kwa hiyo tukafuata ushauri wao na sasa umetusaidia," alisema Fatma Muya mmoja wa walengwa kutoka Mtaa wa Kileleni Kata ya Kibaoni, Handeni.

"Kwa hiyo kwa mimi binafsi nina ng'ombe wawili, mbuzi nane, na ninauza mboga za majani na nimejenga nyumba nikaezeka na bati ya vyumba viwili vya kulala."

Kwa upande wake, Dorkas Mganga, mkazi wa Kidereko alisema yeye alianzisha biashara ya kuuza mboga za majani, ufugaji wa mbuzi pamoja na kilimo cha biashara ya kunde na choroko.

"Kwa hiyo nikipata pesa ya TASAF nikishatoa ya matumizi ya watoto shuleni, nawapatia watu kidogo wanisaidie kulima shambani na kuboreshea biashara zangu ndogo," alisema Mganga.

"Kwa hiyo TASAF imenikomboa sana na mimi kwa sasa nina onekana mtu katikati ya watu, imenizalishia kilimo, biashara ya boga, ufugaji wa kuku, tunapata milo mitatu, watoto wanapata mahitaji yao ya shule na kama unavyoona nimejenga nyumba yangu."



Mkaguzi wa Jeshi la Polisi Kitengo cha Dawati la Jinsia, Analyse Desdery, akitoa mafunzo kwa timu ya waandishi wa habari 15 wanaotekeleza mradi wa nafasi ya vyombo vya habari katika kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa ufadhili wa Mfumo wa Wanawake Tanzania (WFT), jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Gereza lapata maji baada ya miaka 48

**Na Deogratius Nsokolo,** KIBONDO

BAADA ya miaka 48 tangu kuanzishwa kwa Gereza la Wilaya ya Kibondo mkoani Kigoma, hatimaye limepata maji ya uhakika.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) kukabidhi mradi wa maji utakaohudumia gereza la makazi ya watumishi pamoja na wananchi wanaoishi jirani na gereza hilo.

Mkuu wa Gereza la Wilaya ya Kibondo, Mrakibu Mwandamizi wa Magereza, Solomon Mwambingu, alisema kwa muda mrefu hwakuwa na maji ya uhakika na watumishi wamekuwa wakihangaika kutafuta maji na kwamba sasa shida hiyo imekwisha.

Mwambingu aliishukuru UNHCR na serikali kwa mchango wake mkubwa katika kuhakikisha wanaondokana na shida ya maji katika gereza hilo lililoanzishwa mwaka 1974.

Mwakilishi wa Mkuu wa shirika hilo wilayani Kibondo, Benon Odora, alisema shirika hilo litaendelea kusaidia maendeleo ya wananchi kwa kujenga miradi mbalimbali kwa kuwa wilaya hiyo ina mchango mkubwa katika kuwapokea na kuwahifadhi wakimbizi.

Alisema wakati wa makabidhiano ya mradi wa maji kuwa pamoja na kwamba rasilimali ni chache, lakini ni muhimu kusaidia wananchi na hasa katika miradi ya maji na usafi wa mazingira ambayo inatoa hakikisho la wananchi kuwa na afya njema.

"Ukiwa na majisafi, ukiwa na mazingira safi, vyoo, huo ni msaada mkubwa ambao unakwenda kuwakinga wananchi na magonjwa mbalimbali, hivyo wanakuwa na uwezo wa kuchangia maendeleo yao na Taifa," alisema Benon.

Naye Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira wilayani Kibondo, Mhandisi Constantine Shija, alisema mradi huo uliogharimu zaidi ya shilingi milioni 290 utahudumia zaidi ya wananchi 6,000 wa Mtaa wa Nengo jirani na gereza la wilaya pamoja na kuhudumia gereza hilo. Alisema mradi huo umefadhiliwa na UNHCR kwa asilimia 71 na asilimia 29 imefadhiliwa na Shirila la Umoja wa Mataifa la Makazi ambapo utekelezaji umefanywa na mashirika ya Norwegian Refugee Services na TCRS.

Alisema baada ya kukamilika kwa mradi huo RUWASA kwa kushirikiana na wananchi itaunda bodi ya watumiaji maji ili kusaidia utunzaji wa mradi huo ambao unatumia umeme jua katika kuzalisha maji.

Mkuu wa Wilaya ya Kibondo, Kanali Aggrey Magwaza, amewataka wananchi kutunza vyanzo vya maji ili maji yaweze kuwahudumia kwa muda mrefu.

Alisema uharibifu wa vyanzo vya maji umekuwa ni tishio kutokana na shughuli za kibinadamu zinazoendelea.

Akizungumzia wakimbizi alisema wilaya hiyo ambayo ina zaidi ya wakimbizi 100,000 wa Burundi wanaohifadhiwa katika kambi ya Nduta itaendelea kushirikiana na mashirika yanayohudumia wakimbizi ili kuleta ustawi wa wakimbizi na jamii ya Kibondo.

# Hakimu: Njoo mjifunze sheria Wiki ya Sheria

**Na Neema Hussein,** KATAVI

HAKIMU Mkazi Mwandamizi Mfawidhi Mkoa wa Katavi, Gway Sumaye, amewataka wananchi wa mkoa huo kufika katika maadhimisho ya Wiki ya Sheria ili waweze kujua sheria za makosa mbalimbali na kutatuliwa matatizo ya kisheria yanayowakabili.

Akizungumza katika uzinduzi wa Wiki ya Sheria ambayo kimkoa inafanyika katika Manispaa ya Mpanda, Hakimu Sumaye alisema wananchi wasisubiri mpaka wapate kesi ndio wafike mahakamani na kutokujua wapi pa kuanzia.

Aidha, alisema Mahakama ya Wilaya Mpanda kwa mwaka uliopita 2021 imeripoti kesi za jinai 237 kati ya hizo kesi zilizoisha ni 169.

Sumaye alisema, wamejipanga kutoa elimu kwa wiki nzima huku wakiangazia zaidi sheria ya mirathi, migogoro ya ardhi, taraka, migogoro ya ndoa, kesi za mikataba na kesi nyinginezo.

"Wananchi waje waone nini maana ya mahakama mtandao na matumizi ya TEHAMA mahakamani... dhana hii ni muhimu wananchi wakaifahamu vizuri mapema zaidi kwa mafano, sisi sasa hivi mahakamani kesi zote tunasajili kwa mtandao kwa hiyo ni vizuri mkaona mahakama ilivyo sasa," alisema Sumaye.

Kwa mujibu wa mgeni rasmi ambaye alikuwa mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Mpanda, Geofrey Mwashitete, alisema elimu ya kisheria itasaidia kupunguza ajali mbalimbali zinazosababishwa na vyombo vya moto.

Mwashitete alisema, maadhimisho ya Wiki ya Sheria yanakwenda sambamba na zoezi la utoaji elimu kwa umma ili kutimiza dhamira ya mahakama ya Tanzania ya kutoa huduma bora za haki zinazo mlenga mwananchi kama ilivyoainishwa kwenye ibara ya nane ya katiba.

"Nimeambiwa kuwa mahakama imejipanga kushirikiana na wadau mbalimbali kutoa elimu kwa jamii kuhusu mambo yafuatayo, kwanza jukumu la msingi la utoaji haki, pili mpango mkakati na maboresho ya mahakama mtandao, tatu wajibu na mipango ya mahakama na wadau kushiriki zama za mapinduzi ya nne ya viwanda na kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua," alisema Mwashitete.

Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yatadumu kwa muda wa siku saba huku yakiwa na kauli mbiu "zama za mapinduzi ya nne ya viwanda, safari ya maboresho kuelekea mahakama mtandao".

Nipashe
# TESA
Jumanne Januari 25, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

## Kutupa chakula ni 'balaa' zingatia haya kukinusuru



Ukurasa 13



KUELEKEA MKUTANO NCHI MASKINI DOHA

ELIMU

**NA SABATO KASIKA**

WOGA, CHUKI HISABATI

# Wadau: Itapendeza zaidi ikifundishwa kwa vitendo

• Sharti kuweka viboko kando

WANAFUNZI wa shule za msingi na sekondari kwa idadi kubwa hawapendi hisabati, hali inayoelekea kuwa homa ya taifa inaweza kuitwa 'Mathe phobia' (Mathefobia).

Chuki au hofu dhidi ya hisabati, ni tatizo kubwa linasema Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), kuwa wanafunzi wamezidi kufeli na matokeo ya kidato cha nne yaliyotangazwa hivi karibuni watahiniwa wameboronga, ufaulu ukiwa chini ya wastani wa asilimia 19.

Baadhi ya wanafunzi wanaozungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam wanataja sababu zinazosababisha kuichukia hesabu kuwa ni pamoja na somo kujaa kanuni au fumula nyingi, kukosa mbinu mahususi za kukokotoa, mazingira ya kujifunzia si ya kuwavutia, lakini uwezo wa walimu kuwasaidia wanafunzi kupenda hisabati si mkubwa.

Daniela Mosha wa Shule ya British ya Mwenge, anaeleza kuwa walimu wa hisabati walioko hawana uelewa mkubwa wa somo hilo na hata wachache wanaolielewa hufundisha wanafunzi wengi pengine kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne hali inayopunguza ufanisi, ikiwa ni shida wanayoipata pia walimu wa bailojia, kemia na fizikia. Yote hayo huchangia kufanya ufaulu wa hisabati kuwa duni.

"Kutokana na 'mathefobia' wanafunzi wengi wanapendelea kusoma michepuo ambayo haina hisabati, wanakimbilia masomo ya sanaa. Ni kwasababu hisabati inaweza kutukwamisha kuendelea na masomo ya kidato cha tano na sita na kufikia elimu ya juu." Anasema Aden Mbura wa Mbezi High School.



Mwenyekiti wa Jukwaa la Sera la Chama cha Wamiliki wa Shule Binafsi , Benjamin Nkonya, akizungumza na wadau wa elimu. **PICHA: SABATO KASIKA**

Akizungumzia sababu za kuchukua hesabu na mbinu za kuongeza ufaulu, Mwenyekiti wa Jukwaa la Sera la Chama cha Wamiliki wa Shule Binafsi (TAMONGOSCO), Benjamin Nkonya, anasema, sababu za wanafunzi kufanya vibaya ni ukosefu wa mbinu za ufundishaji.

"Tatizo ni kukazania ufundisha nadharia na kuweka pembeni vitendo, hali ambayo inasababisha wanafunzi washindwe kuelewa kwa urahisi somo hilo," anasema Nkonya.

Anatolea mfano kuwa ili mwanafunzi aelewe vizuri umbo la pembe tatu au 'skwea', ni vyema hata akapelekwa kwa mafundi seremala aone jinsi zilivyo badala ya kufundishwa kwa nadharia muda wote.

"Kukiwa na utaratibu huo wa ufundishaji wa njia ya vitendo, itakuwa ni rahisi wanafunzi kuelewa somo hilo, lakini tukiendelea na utaratibu wa sasa wa kutotenga bajeti kwa ajili ya vitendo, hatuwezi kupiga hatua," anasema.

Anasema, wanafunzi wengi siku hizi wanasoma masomo ya ziada, lakini bado wanafanya vibaya kwenye somo hilo, na kwamba sababu kubwa ni hiyo ya ukosefu wa masomo kwa njia ya vitendo.

"Hebu fikiria, mwanafunzi aliyefanya vibaya katika somo hilo, akipewa kazi ya kuuza duka anafanya vizuri, akiwa kondakta wa daladala anarudisha chenji vizuri. Hii ina maana kwamba ufundishaji wetu una tatizo," anasema.

Anasema, umefika wakati sasa kuangalia umuhimu wa ufundishaji wa njia ya vitendo, ili kuwajengea wanafunzi uelewa zaidi wa somo hilo. Kwa madai kwamba wanaliweza ila wanakwamishwa na mbinu za ufundishaji.

**WASIWE WAOGA**

Mwalimu wa Chuo Archbishop University College of Tabora (AMUCTA), Dennis Mwiga, anasema kujengeka tabia ya kuchukia na kuogopa hisabati, walimu wa somo kuwa wachache na mtaala kutokuwa sawa na mfumo wa maisha ya wanafunzi vinachangia

"Ukiangalia mtaala, utagundua kuwa una vitu vingi ambavyo

INAENDELEA UK.14

ELIMU

**NA MWANDISHI WETU**

# Kutupa chakula ni 'balaa' zingatia haya kukinusuru



Watu wasio na chakula wakisaka vyakula majalalani.Hali hiyo inalazimisha kujua umuhimu wa kutunza na kuenzi chakula na hata kuwasaidia wasio nacho. **PICHA: MTANDAO**

> **Kupunguza upotevu na utupaji wa chakula ni muhimu katika dunia ambayo mamilioni ya watu wanalala njaa kila siku.**



KUTUPA chakula ovyo kama ugali, wali na mboga za aina mbalimbali ni jambo la kawaida mijini hasa kwenye majiji kama Dar es Salaam na Dodoma.

Majalala ya maeneo ya makazi yanajaa vyakula, tena si jambo geni kukuta mapande ya ugali yamemwagwa karibu na nyumba, mengine yamerundikana kwenye viroba vya taka pembeni ya barabara, huku wali na ukoko wake ukitapakaa ovyo. Wanaoona wanajiuliza kwani wanaotupa hawajui kukadiria au kupima chakula?

Utupaji wa chakula si jambo jema. Usitupe chakula kibichi wala kilichopikwa uwe muuzaji dukani, mama na baba lishe, mfanyabiashara na mkulima, acha.

"Kupunguza upotevu na utupaji wa chakula ni muhimu katika dunia ambayo mamilioni ya watu wanalala njaa kila siku," linasema Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa -FAO.

FAO inasisitiza: "Tunapopunguza kutupa chakula, tunaheshimu kuwa chakula hakipatikani kirahisi kwa mamilioni ya watu ambao wanalala njaa kila siku. Ni juu yetu sote kubadili tabia zetu ili kufanya upotevu wa chakula kuwa ndiyo mfumo wa maisha yetu."

Ili kufikia azma ya kutunza chakula FAO inaainisha hatua rahisi ambazo kila mmoja anatakiwa kuzichukua ili kukithamini na kukienzi chakula ambacho hakipatikani kwa urahisi na si kila mtu anakula au kunywa.

Kuna watu ambao hawafurahii matunda, mboga, nyama za aina mbalimbali na samaki. Wapo mamilioni duniani pamoja na Watanzania ambao hawapati chakula wala hawafahamu watakula nini na wamedhoofu.

**UNACHOSHAURIWA**

FAO inashauri kupika chakula kinachotosha mahitaji ya walaji, pia kupakua chakula kiasi kidogo. Usipakue sahani iliyojaa tele hata ukashindwa kuimaliza. Chukua kidogo ukihitaji tena ongeza. Ukishiba kwa kiasi ulichochota inafaa kwa sababu umetunza chakula.

Aidha, inaelekeza kutumia lishe bora na endelevu. Hii inamaanisha kuishi maisha yanayoenda kwa kasi na kuandaa chakula chenye lishe inaweza kuwa changamoto, lakini milo yenye afya si lazima itumie muda kuandaliwa. Mfano samaki au dagaa, mboga za majini kama kabichi, mchicha, spinachi na ugali au wala, tambi, chapati, ndizi, mihogo. Vinaandaliwa haraka na huiva kwa muda mfupi. Wakati mwingine ni vyema kuloweka vyakula vigumu kama mahindi na maharage au kutumia teknolojia ya kupika kwa mvuke ili kuokoa moto mwingi au nishati kubwa inayotumika kuviivisha.

FAO inashauri watu kununua kile wanachohitaji na kuhimiza kupanga chakula kwa kuandaa orodha ya mambo ya kununua na kuizingatia ili kuepuka kununua kwa kukurupuka.

Ukinunua chakula unachohitaji utaepuka kupoteza chakula kidogo, bali pia utaokoa pesa yako, unayoitumia kununua vyakula vingi ambavyo mwishoni vinaharibika.

Usiyakimbie matunda na mboga zenye mwonekano mbaya, pia usihukumu chakula kwa mwonekano kwake. Matunda na mboga zenye umbo la kushangaza au zilizopondeka mara nyingi hutupiliwa mbali kwa sababu hazifikii viwango vya kupendezesha macho ya wateja.

Ni vyema kuvinunua pia kwani ladha yake ni ileile. Tumia matunda yaliyokomaa kwa kuyatengeneza juisi na kuyala, inashauri FAO.

Kuhifadhi chakula kwa utaratibu unaofaa kwenye friji ni jambo linalosisitizwa na FAO. Inawashauri kusogeza bidhaa za zamani mbele kwenye friji au ndani ya kabati na vipya viwekwe nyuma ili vya zamani, vionekane na kutumiwa.

Lakini ili kuzuia chakula kisiharibike ndani ya friji watu wanashauriwa kutumia vyombo visivyoingiza hewa kuwekea vyakula hivyo na kuvifunga ili kuzuia wadudu kuingia na mwisho kuharibu na kutupa chakula kwa uzembe. Kuielewa dhana ya tarehe ya kuharibika (expiry date) ili kufahamu kuweka chakula mpaka lini? Kuna tofauti kubwa kati ya tarehe "bora kabla ya kuharibika " na "matumizi yafanyike hadi lini."

Wakati mwingine chakula bado ni salama kula baada ya tarehe isemayo "bora kabla ya... expiry date ", lakini ni muhimu kuweka tarehe isemayo "matumizi yaishe ifikapo" ambayo inakuambia wakati na mwisho wa kutumia au chakua hicho, au si salama tena kuliwa.

Unashauri kutunza mabaki yako na endapo hutaweza kula kila kitu, kihifadhi kilichosalia kwenye jokofu kwa ajili ya baadaye au tumia kilichobaki kuandaa mlo mwingine, kama ugali au uji wa mchele usitupe vilivyobakia. Ni vizuri kuheshimu chakula, ambacho huwaunganisha watu wote duniani.

Jifunze na jua mchakato wa kuandaa chakula. Ni vizuri pia kusoma na kujua uzalishaji wa chakula na uwajue wakulima wanaozalisha chakula hicho kwa mfano ugumu wa kuzalisha viungo kama vanila.

Changamoto wanazopitia wakulima wakati wa kuandaa mashamba, kulima mpunga kuuchakata na kuufikisha sokoni.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Kuelekea mkutano nchi maskini

• Nyavu zinazoinasa Afrika kiteknolojia



Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni ya kisasa na ya kwanza Afrika iliyojengwa na China ikiwa ni msaada wa miradi inayohusisha matumizi ya teknolojia kwenye elimu. **PICHA: MTANDAO**

WAKATI wowote kuanzia sasa viongozi wa Afrika, Umoja wa Mataifa (UN), mataifa tajiri duniani maarufu G8 na wadau wengine wanatarajia kushiriki mkutano wa UN , mahsusi kwa ajili ya nchi maskini duniani, utakaofanyika Doha nchini Qatar.

Ni tukio linalofanyika kila baada ya miaka 10 likiandaliwa na ofisi ya UN inayoshughulika na mataifa maskini, visiwa vidogo na nchi zisizo na bahari ambazo zote ziko duni kiuchumi na watu wake wanaishi bila kuwa na uhakika wa chakula, matibabu, elimu bora na bajeti zao zinategemea misaada na mikopo ya mataifa tajiri kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Kongamano hilo ni muhimu kuangalia makubaliano na mipango iliyowekwa wakati wa mkutano wa nchi maskini uliofanyika Istanbul mwaka 2011, kuweka mikakati mingine na kujipanga upya kwa ajili ya kusonga mbele lengo likiwa ni kuzisaidia nchi maskini kuondokana au kufuta sifa ya umaskini na 'kubatizwa' mataifa yaliyoendelea' ifikapo 2030 kwa vile yamebakia na sifa hiyo kwa miongo mingi tangu uhuru hadi sasa.

Baadhi ya nchi maskini ni mataifa yaliyoko Kusini ya Jangwa la Sahara kama Tanzania, Angola, Benin, Burkina-Faso, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Kenya, Rwanda na visiwa vya Sao Tome na Principe.

Mengine ni nchi za Asia kama Afghanistan, Bangladesh, Jamhuri ya Lao, Myanmar, Cambodia, Nepal na Bhutan. Aidha, mataifa maskini mengine ni Haiti iliyoko Bara la Amerika na visiwa vya Kiribati vilivyoko kwenye Bahari ya Pasifiki.

Pamoja na mkutano huo kuahirishwa kwani ulikuwa ufanyike kuanzia Jumapili iliyopita Januari 27, Afrika ambayo ni bara lenye kundi kubwa la nchi maskini zaidi ya 34, inapojitazama inazidi kukwama kwenye eneo la teknolojia, licha ya kujinasibu kuwa inahitaji kuitumia ili kujiletea maendeleo katika karne ya 21.

Umoja wa Afrika unaamini kuwa teknolojia ni muhimu kukabiliana na changamoto zitokanazo na zama za kidijitali zinazofanikishwa na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHEMA), kwani ina nafasi ya pekee kwenye maendeleo na uti wa mgongo wa uchumi viwanda wakati ikielekea kuwa bara lenye uchumi wa viwanda kabla ya 2030.

> **Ni kwa sababu hakukuwa na uwekezaji, mradi ulikuwa na wafadhili walivyoondoka hakukuwa na mwendelezo.**

Wakati mkutano wa Doha ukisubiriwa, makala hii inaitazama hali ya Afrika yenye idadi kubwa ya watu maskini na mataifa yao hayaondoki kwenye umaskini licha ya kusaidiwa kwa miaka mingi, kufikia maendeleo ya teknolojia.

Nipashe inazungumza na Wakati Mwaruka, Meneja wa Karakana ya Kituo cha Ubunifu na Uhawilishaji wa Teknolojia (TDTC) cha Shule Kuu ya Uhandisi (COeT) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kuhusu sababu za kudidimia badala ya kuinuka kwa bara hilo kiteknolojia....

***SWALI: Unadhani ni sababu zipi zinazoikwamisha Afrika kwenye maendeleo ya teknolojia?***

***JIBU:*** Haiendelei kwa sababu nyingi lakini, kubwa ni kukosekana kwa ridhaa ya kisiasa ya kuwekeza fedha za kutosha kuendeleza teknolojia kwa mataifa mengi maskini. Mfano Afrika ina wataalamu, wasomi na wabunifu walioko kwenye vituo vya teknolojia duniani kama kile cha anga za juu cha Marekani -NASA.

Si hivyo tu, wapo mabingwa wakiwamo madaktari na wagunduzi ambao badala ya kuhudumia Afrika wako ughaibuni kwa sababu serikali hajaweza kuwekeza, kuthamini wala kufuatilia masuala ya ubunifu na utafiti wanayogundua au kuibua.

Wameondoka kwenye nchi zao kwasababu wameona kuwa hata wakibuni na kugundua teknolojia hawafiki mbali. Ukigundua teknolojia hufiki mbali kwasababu huwezi kuiendeleza, inahitaji kuiboresha na kuifikisha mbali ikiwamo kutumia kuzalisha huduma na bidhaa kutatua changamoto kwenye jamii.

SWALI: Tupe mifano. Nitoe mfano, kuna wakati Tanzania ilikabiliwa na uhaba mkubwa wa sukari na wataalamu waligundua teknolojia ya uzalishaji sukari kwa teknolojia rahisi kwenye mashamba ya miwa. Haikufika mbali iliishia kwenye hatua za ugunduzi, na hata leo uhaba wa sukari unatokea, ikiagizwa kutoka nje.

Ni kwa sababu hakukuwa na uwekezaji, mradi ulikuwa na wafadhili walivyoondoka hakukuwa na mwendelezo.

Ndivyo ilivyokuwa kwa mashine za kukamua mafuta ya michikichi yanayozalishwa Kigoma. Ni moja ya miradi iliyobuniwa na kuendelezwa na wataalamu kukabiliana na upungufu wa mafuta nchini, lakini kwa sababu ya kukosekana uwekezaji haukufanikiwa na hata sasa changamoto za uhaba wa mafuta hazijakwisha. Kinachokwamisha ni serikali za Afrika hazijaona umuhimu wa kuwekeza kwenye maendeleo ya teknolojia na utafiti kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

***SWALI: Eneo jingine linalokwamisha maendeleo ya sayansi na teknolojia ni ipi?***

***JIBU:*** Kukosekana kwa mashine na mitambo ya kuzalisha bidhaa za kiteknolojia. Kwa mfano miaka ya 1980 vilianzishwa vituo vingi vya teknolojia kama Nyumbu ya Jeshi la Wananchi, kushughulika na uzalishaji wa magari. Lakini hatuoni magari yao barabarani yanaonekana kwenye maonyesho kama Sabasaba lakini sio sokoni yakiuzwa au barabarani yakifanyakazi.

Kulikuwa na kituo cha kuendeleza teknolojia za kilimo kwa ajili ya kuboresha uzalishaji mashambani (Centre for Agricultural Mechanization and Rural Technology (CAMARTEC), si hivyo hata UDSM kulikuwa na Taasisi ya IPI, Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda (TIRDO) vyote hivyo havikuweza kuendelezwa,

**INAENDELEA UK.14**

# Kuelekea mkutano nchi maskini

INATOKA UK.13

havikupata uwekezaji wa kutosha, wala mitambo ya kuzalisha bidhaa na teknolojia matokeo yake taifa halijaweza kunufaika kikamilifu na vituo hivyo.

Kama taasisi za Afrika hazipati wafadhili wanaotoa fedha na kugharamia mitambo na mashine kazi za teknolojia, inakuwa vigumu kuziendeleza kwa vile bado serikali hazijaona umuhimu huo wala kuweka nia ya dhati ya kisiasa ya kufanyakazi ya kuliimarisha eneo hilo.

***SWALI:* *Unazungumziaje ajira za wataalamu wa sayansi?***

***JIBU:*** Nadhani, serikali nyingi za Afrika haziwekezi kusomesha wala kuajiri wanasayansi, watafiti na wabunifu wa teknolojia. Ndiyo maana sekta ya sayansi inakabiliwa na changamoto kama madaktari bingwa, wahandisi wa mitambo, mainjinia wa simu, TEHAMA, kama 'waya less', madini, viwanda vya vyakula, umeme na dawa.

Wataalamu hao hawaajiriwi, lakini pia hakuna karakana za kisasa za utafiti zenye wabunifu wa masuala ya teknolojia na utafiti hivyo inakuwa vigumu kuwa na maendeleo kwenye sekta hiyo.

Kama hatuajiri mainjiania, wanasayansi, watafiti, wabunifu na hakuna maabara na vituo vikubwa vya kufanyakazi hizo inakuwa vigumu kuendelea na kubadilika kiuchumi kwa vile kila hatua ya maendeleo ni lazima ianzishwe na teknolojia kutoka ngazi za chini kwenda za juu.

***SWALI: Unadhani mataifa yaliyoendelea yanaweza kuwa chanzo cha kukwamisha nchi maskini kwenye maendeleo ya teknolojia?***

***JIBU:*** Ni maoni yangu sivyo. Ni kwa sababu Afrika imesaidiwa sana kukuza teknolojia kwa mfano binafsi nilishiriki kwenye mafunzo ya kuzalisha teknolojia ya umeme wa maji ambayo ingekwenda vijijini.

Yaliyofanikishwa na Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (UNIDO), tukienda Indonesia, tulifunzwa na kuiva kwenye kutengeneza teknolojia hiyo na tuliporudi nyumbani kuihawilisha tulikwama kwa vile tulitakiwa kuwekeza, lakini mradi huo uliohusisha nchi maskini haukufanikiwa sehemu kwa sababu serikali hazikuuendeleza baada ya UNIDO.

China imeisaidia Tanzania imejenga maktaba ya kisasa ya kwanza barani Afrika kwa teknolojia bora na uwezo wa kuhifadhi vitabu zaidi ya 800,000 ikiwa ni moja ya maktaba bora duniani, inayounganishwa na kompyuta zenye mitandao ya mawasiliano ya kimaktaba.

Mataifa yaliyoendelea yamesaidia na kwa mfano wa maktaba hiyo, ni jukumu la wataalamu wetu TEHAMA, kusambaza teknolojia ya maktaba hiyo kwenye vyuo vikuu vingine nchini.

> **"Hili linathibitishwa na baadhi ya mataifa kama Rwanda yameanzisha miradi ya kiteknolojia ya kuunda magari.**

UFUMBUZI

***SWALI: Unazungumziaje kuhusu ufumbuzi wa tatizo hilo?***

***JIBU:*** Ni lazima mataifa maskini yenyewe yaanze kujitambua na kubadilika na kuwekeza kwenye teknolojia na fedha za miradi ya 'risechi', ubunifu na ugunduzi pamoja na kuendeleza utaalamu wetu wenyewe zitoke ndani ya hazina za mataifa yetu.

Si jambo rahisi nchi zilizoendelea zikaja kuwekeza kwenye utafiti, teknolojia na kutufundishia wataalamu kwenye mataifa yetu. Ni sisi wenyewe tuwe mstari wa mbele. Ndiyo maana inahitajika ridhaa ya kisiasa kufanya hivyo.

Hili linathibitishwa na baadhi ya mataifa kama Rwanda yameanzisha miradi ya kiteknolojia ya kuunda magari ya Volkswagen Kigali, kufuatia juhudi kubwa ya viongozi wakuu wa kisiasa.

Nchi maskini ziwekeze kwenye taasisi za kitafiti, ubunifu na ugunduzi kwa pamoja kutumia fedha zao wenyewe badala ya kuangalia wahisani.

Vituo hivyo vibuni teknolojia rahisi na nafuu kuboresha kilimo, nishati, ufugaji, usafiri, kuongeza thamani mazao na bidhaa za viwandani ili tutoke kwenye kundi maskini na kuingia kwenye ngazi ya watu wenye maendeleo.

Kama hatutaamua kubadilika tutaendelea kubakia kama tulivyo miaka yote na Afrika haitaondoka kwenye kundi la nchi maskini na kuingia kwenye mataifa yaliyoendelea kiviwanda.



Teknolojia duni ya upishi wa kutumia mawe matatu bado inatawala majiko ya familia nyingi za Afrika. Moshi huchafua mazingira lakini kuni na mkaa inamaliza misitu. **PICHA: MTANDAO**

# Wadau: Itapendeza zaidi ikifundishwa kwa vitendo

INATOKA UK.11

havina umuhimu katika maisha ya kila siku," anasema Mwiga.

Umefika wakati kuangalia uwezekano wa kuwaondolea wanafunzi dhana kwamba somo hilo ni gumu, kupunguza vitu ambavyo si vya muhimu kwa maisha ya sasa katika mtaala.

"Pamoja na hayo, kuna haja ya kuongeza idadi ya walimu wa somo hilo, kuweka msukumo zaidi kwenye hisabati. Kwa maana kwamba somo lipewa kipaumbele kuanzia shule za awali," anasema.

Hisabati imepewa majina mengi kama 'baba mkwe au ugonjwa wa taifa', ni kutokana na dhana iliyoko vichwani mwa baadhi ya wanafunzi kuwa ni ngumu.

"Ninaamini kwamba, dhana hiyo ikiondoka, kukawa na walimu wa kutosha wa, kupunguza baadhi ya vitu kwenye mtaala na kukawa na mkakati maalum wa kuimarisha somo hilo, tutapiga hatua," anasema.

**KUACHA VIBOKO**

Kamishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mutahabwa, anasema amefuatilia baadhi ya shule na kukuta, mwalimu anapowapa wanafunzi hesabu 10 anakuwa na mzigo wa fimbo, atakayekosa hesabu tano atapata viboko vitano, akishindwa tatu atachapwa fimbo tatu.

"Unapigwa fimbo kulingana na idadi ya hesabu ulizokosa. Endapo kuna mwalimu mwenye dhana kwamba anapofundisha akitumia fimbo inasaidia kumjaza akili mwanafunzi, atakuwa anajidanganya, ualimu hauko hivyo," anasema Dk. Mutahabwa anaiambia Nipashe kwenye mahojiano.

Anawashauri walimu wanaofundisha somo hilo kuwa na ushirikiano, upendo na kuwa tayari wakati wote kuwasaidia wanafunzi, kwamba kwa kufanya hivyo, wanafunzi wengi watafaulu.

"Utafiti unaonyesha kuwa ili mwanafunzi azingatie masomo ya mwalimu anayemfundisha, ni lazima kuwapo na upendo na heshima kati yao ili miaka ijayo mwanafunzi huyo atamani kuwa mwalimu," anasema.

Aidha, Dk. Mutahabwa anasema, iwapo mwanafunzi atampenda mwalimu anayemfundisha, atalipenda pia somo husika analofundishwa na kulisoma mara kwa mara kutokana na urafiki uliojengeka.

"Kipindi chako hatakikosa, lakini ukiwa mwalimu uliyejaa matusi, ubabe, dharau, dhihaka, kashfa, vitisho na mzigo wa fimbo pembeni usitegemee kufanikiwa," anasema.



# Tume ya Utumishi Mahakama yafundwa

**Na Renatha Msungu** DODOMA

JAJI Kiongozi Mustapha Siyani, amewataka watumishi wa Tume ya Utumishi ya Mahakama kuacha kufanya kazi kwa mazoea badala yake wafanye kwa nguvu ili kuwatumikia wananchi ipasavyo.

Akizungumza wakati akifungua Baraza la Wafanyakazi wa Tume hiyo juzi, Jaji Sian alisema watumishi wa tume hiyo hawapaswi kuchukulia mazoea ya utendaji kazi zao kinachotakiwa ni kujituma ili kuwatumikia wananchi kwa ufasaha.

"Nawaomba mkafanye kazi kwa bidii acheni kuendekeza mazoea yatawaharibia kazi zenu za kila siku,"alisema Jaji Sian.

Alifafanua kuwa mahakama ni sehemu ya watu kupata kazi, hivyo watumishi hawatakiwi kuleta mzaha katika utoaji haki za jamii pale wanapohitajika.

Alisema hakuna taasisi ambayo haiangalii suala la nidhamu hivyo wanapaswa kusimamia nidhamu ili kazi zao zionekane bora katika kila sehemu wanapokwenda kufanya kazi zao mbele ya jamii.

Naye Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Prof. Elisante Ole Gabriel, alisema Baraza la Watumishi ni chimbuko la tamko la Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere la mwaka 1970, na limeundwa kwa ajili ya kuwashirikisha wafanyakazi katika mambo mbalimbali.

Alisema toka lilipoanzishwa bado jitihada zinaendelea kwa ajili ya kuwapata wafanyakazi katika baraza hilo ambao watakuwa wakishiriki kwa ajili ya kutoa kero zao.

Alisema Tume ya Mahakama ina upungufu wa watumishi, hivyo wanahitaji watumishi 15 kwa ajili ya kuziba mapengo mbalimbali.

Katika hatua nyingine Prof. Elisante alizishukuru kamati za halmashauri na mikoa ambazo zimekuwa zikikutana mara kwa mara kupanga mafunzo ya wajumbe wa tume hiyo.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni pamoja na kuwekana sawa wajumbe, lakini wao watakwenda uwaweka sawa jamii kwa kuwapa elimu.

Alisema limetengwa fungu kwa ajili ya kwenda kutoa elimu katika mikoa ya Dodoma, Singida, Morogoro, Shinyanga na Simiyu.

# Wataalamu 400 wanolewa mfumo wa anuani za makazi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetoa mafunzo ya utekelezaji wa mfumo wa anuani za makazi kwa wataalamu zaidi ya 400 wa mikoa na halmashauri Tanzania Bara na Zanzibar watakaosaidia kufikia azma yake ya kukamilisha mfumo huo kabla ya Mei, 2022.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Jim Yonazi, akizungumza juzi wakati wa kufunga mafunzo hayo kwa njia ya mtandao, alisema wataalamu hao wanakwenda kuisaidia serikali kufikia azma ya kukamilisha utekelezaji wa mfumo kabla ya Mei, 2022.

"Katika hili nitoe wito kwa viongozi na waratibu wa mradi huu katika ngazi ya wizara zinazotekeleza kuhakikisha wanakuwa bega kwa bega na wataalamu hawa waliohitimu leo katika kutatua changamoto mbalimbali zitakazojitokeza wakati wote wa utekelezaji wa zoezi hili.

"Tulianza mafunzo haya mnamo tarehe 17 Januari, 2022 na leo tunakwenda kuhitimisha, ni takribani siku 7 ambazo mmejengewa uwezo juu ya anwani za makazi ni matumaini yangu kwamba mmeelewa vizuri mlichofundishwa na sasa mko tayari kuanza utekelezaji wa mfumo wa anwani za makazi kila mmoja katika eneo lake,"alisema.

Aidha, alisema ni matumaini ya viongozi pamoja na serikali kwa ujumla kuwa sasa wamepatikana wataalamu mahiri wenye ufanisi wa hali ya juu kuhusu mfumo wa anuani za makazi.

"Nafahamu kwamba wengi wenu mnatoka katika halmashauri ambazo pengine nyie ndio watendaji mnaotegemewa zaidi katika ofisi zenu, jambo la anwani za makazi ni jambo la kitaifa lenye maelekezo na lina ukomo wa utekelezaji.

"Kwa msingi huo nitumie fursa hii kuwaelekeza wakurugenzi wa halmashauri zote nchini, kuwaondolea majukumu mengine wataalamu waliopatiwa mafunzo katika kipindi hiki ambacho tunaendelea na utekelezaji wa mfumo wa anuani za makazi ambao kimsingi wataalamu hao ndio waratibu wa utekelezaji katika maeneo yao,"alisisitiza Yonazi.

Alisema ni wazi kuwa halmashauri zina kazi nyingi ambazo zote ni muhimu, lakini anaomba walipe kipaumbele suala hilo ili kufikia malengo tarajiwa.

Kadhalika alisema wataalamu hao ndiyo wabeba maono, wanaokwenda kuandika historia mpya ndani ya taifa katika kuhakikisha nchi inakuwa na mfumo imara na thabiti wa utambuzi.

Hata hivyo, aliwaomba wakayatumie vyema maudhui ya mafunzo waliyoyapata katika kufanikisha utekelezaji wa mfumo huo kwenye maeneo yao ndani ya muda uliopangwa.

Vilevile, alisema wizara yake itakuwa tayari kushirikiana nao pale itakapohitajika ili kufanikisha utekelezaji.

"Aidha, nitapenda kupata taarifa ya utekelezaji kila baada ya wiki mbili kutoka katika halmashauri zenu kuanzia tarehe ya kuisha kwa mafunzo haya ambayo ni leo tarehe 23 Januari 2022," alisema.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano Taifa, Alhaji Sheikh Mussa Salumu (kushoto), akipongezwa na viongozi mbalimbali baada ya kutunukiwa shahada ya udaktari kwenye mahafari yaliyofanyika mkoani Dodoma, (kulia) Spika mstaafu wa Bunge, Anna Makinda. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Makinda aiomba jumuiya uhamasishaji sensa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KAMISAA wa Sensa ya Watu na Makazi, Spika mstaafu wa Bunge, Anna Makinda, amesema kuwa ni imani yake kubwa viongozi wa Jumuiya ya Maridhiano Tanzania itaisaidia serikali katika kuwahamasisha Watanzania kujitokeza kwa wingi kwenye zoezi la uandikishaji litakalofanyika nchini mwaka huu.

Makinda alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na viongozi na wanachama wa Jumuiya ya Maridhiano mkoa wa Dodoma.

Alikuwa akizungumza kwenye mkutano huo ambao ulikuwa na lengo la kuipongeza serikali ya awamu ya sita katika kuimarisha uchumi na kuendeleza miradi ya maendeleo kwa ajili ya Watanzania.

Makinda alisema kuwa jumuiya hiyo ina nafasi kubwa ya kushawishi na kuwahamasisha watu kujitokeza kwa wingi ili kushiriki zoezi hilo muhimu ambalo kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania kiuchumi.

Alisema kuwa serikali ina imani kubwa kwa jumuiya hiyo katika kushirikiana ili zoezi hilo liweze kufikia malengo yake katika maendeleo ya kiuchumi kwa watu wake.

"Ni imani yangu kubwa kwenu nyinyi viongozi na wanachama wa Jumuiya ya Maridhiano Tanzania, mtaisaidia serikali kama mnavyosaidia shughuli mbalimbali za maendeleo na kuhubiri amani, nayo hata hili la sensa ya watu na makazi lipo mikononi mwenu katika kuhamasisha watu kujiandikisha,"alisema.

Aidha, aliwataka Watanzania pia kutoa ushirikiano katika utoaji wa majibu sasa kwa watumishi watakaoandikisha huko majumbani na maeneo mengineyo, ili zoezi hilo liweze kupata idadi kamili ya watu na makazi yao.

Naye Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, akizungumza kwenye mkutano huo uliojumuisha pia na viongozi wa ngazi mbalimbali wa serikali, alizitaka familia ambazo zina watoto wenye ulemavu kutowaficha katika zoezi la uandikishaji wa sensa ya watu na makazi utakapofanyika mwaka huu.

Alisema kuwa tabia ya kuwaficha watu hao wenye ulemavu itaisababishia serikali kutowatambua watu wake, ikashindwa kufikia malengo yake ya bajeti itakayopangwa kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania na pia inawanyima haki yao ya kimsingi ya kuhesabiwa kama ilivyo kwa watu wengine.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano Taifa, Alhaji Sheikh Mussa Salumu, alisema kuwa lengo kuu la jumuiya ni kuhakikisha amani ya Tanzania inadumishwa na kulindwa kwa gharama yoyote.

Alisema kwa kushirikiana na serikali Jumuiya ya Maridhiano itahakikisha amani inadumishwa kwa dini zote, ili Watanzania waweze kufikia malengo yao kiuchumi na maendeleo.





# Washindwa kupata huduma za kijamii daraja lasombwa

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

WAKAZI wa vijiji sita vya Kata ya Luteba katika Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe, wanashindwa kupata huduma za kijamii kwa zaidi ya miezi sita kutokana na mawasiliano ya barabara kukatika baada ya daraja la Mto Lufilyo kusombwa na mafuriko.

Vijiji hivyo ni Luteba, Isale, Mpunguti, Ikubo, Kilasi na Ipuguso ambavyo wananchi wake wanapata huduma za kijamii katika Kata ya Kandete iliyoko Bonde la Mwakaleli.

Wananchi hao walisema kabla ya daraja hilo kubomoka walikuwa wanatembea kilomita tatu kwenda katika Kata ya Kandete na tangu lilipobomoka wanalazimika kuzunguka umbali wa zaidi ya kilomita 16.

Wakizungumza na waandishi wa habari wananchi hao waliomba serikali iwajengee daraja hilo ili kuwapunguzia tatizo la gharama za usafiri kutoka kwenye maeneo yao kwenda kwenye eneo ambalo huduma za kijamii zinapatikana.

Mmoja wa wananchi hao, Jimmy Mwaitulu, alisema daraja hilo lilisombwa na mafuriko mwezi Mei mwaka jana na waliahidiwa kuwa lingejengwa haraka, lakini mpaka sasa halijajengwa hali ambayo inawatesa.

Alisema kutokana na mzunguko wa njia wanayoitumia kuwa mrefu hata huduma wanazopata zimepanda bei hasa huduma za madukani na kuiomba serikali iwasaidie.

"Tunapata shida kubwa sana kwenye vijiji vyetu, hili daraja ni kiunganishi muhimu sana kwetu sasa tangu lilipOsombwa na mafuriko hatuna mawasiliano ya barabara," alisema Mwaitulu.

Naye Atupele Mwandeko, alisema kabla daraja hilo halijavunjika usafiri wa bodaboda gharama ilikuwa Sh. 3,000, lakini kwa sasa kutokana na mzunguko uliopo wanalipa Sh. 9,000 gharama ambayo alidai ni kubwa na haiendani na kipato chao.

Alisema endapo serikali itawajengea daraja hilo, gharama za usafiri zitapungua na kufikia Sh. 3,000 kama ilivyokuwa zamani na huduma zingine za kijamii gharama zitapungua.

"Tunamwomba sana rais wetu atusaidie kuweka msukumo ili daraja letu likamilike na tuanze kupata huduma muhimu za kijamii, hili daraja ni muhimu sana kwa mawasiliano ya vijiji vyetu na majirani zetu," alisema Mwandeko.

Emmy Mwakilembe, alisema kwa sasa katika kijiji chao kila huduma imepanda na wanawake ndiyo wanaopata shida zaidi kwenye tatizo hilo.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Wilson Charles, alisema katika mto huo yalibomoka madaraja mawili ambayo moja limeanza kujengwa na linalolalamikiwa na wananchi linafanyiwa kazi.

Alisema daraja linalolalamikiwa na wananchi litajengwa kwa kutumia vyanzo vingine vya fedha na sio bajeti ya TARURA.



Baadhi ya wakazi wa Kata ya Luteba katika Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe wakiangalia daraja la Mto Lufilyo ambalo lilibomoka tangu mwezi Mei, mwaka jana na kukata mawasiliano ya kata hiyo na Kandete ambako ndiko wanakopata huduma za kijamii. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## CWT yataka utatuzi migogoro kidiplomasia

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT), kimeahidi kushirikiana na serikali kutatua matatizo ya walimu kidiplomasia badala ya migomo kama ilivyozoeleka.

Katibu Mkuu wa CWT, Mwalim Deus Seif, aliyasema hayo wakati chama hicho kilipokuwa kinakabidhi mifuko 500 ya saruji kwa Serikali ya Mkoa wa Mbeya kwa ajili ya kusaidia kuboresha miundombinu ya elimu mkoani humo.

Alisema kwa muda mrefu walimu wamekuwa wakikabiliana na matatizo mbalimbali, lakini ilikuwa inatumia mbinu ambazo zilikuwa hazisaidii kutatua matatizo hayo na zaidi zilikuwa zinawaumiza wanafunzi.

"Sekta ya elimu ni muhimu sana na ndiyo maana tumeamua kuja na mbinu mpya za kutatua matatizo ya walimu kwa kushirikiana na serikali ili tutatuwe matatizo haya kwa kujadiliana," alisema Seif.

Mwalimu Seif alisema mifuko ya saruji ambayo walikabidhi ina thamani ya Shilingi milioni saba na waliitoa kama sehemu ya kuunga mkono serikali kwenye uboreshaji wa miundombinu ya elimu.

Akizungumza kwa niaba ya wakurugenzi wa Mkoa wa Mbeya, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Renatus Mchau, alisema mifuko ya saruji waliyopatiwa na chama hicho itasaidia kukamilisha baadhi ya vyumba vya madarasa.

Akipokea mifuko hiyo kwa niaba ya serikali, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Angelina Lutambi, alisema walikiomba chama hicho msaada huo muda mrefu kabla hata ya ujio wa fedha za UVIKO-19.

Alisema msaada huo utasaidia kukamilisha baadhi ya miundombinu ya elimu hasa vyoo na madarasa na kwamba serikali inawaalika na wadau wengine kusaidia miradi mbalimbali na sio kwenye elimu pekee.

# Mahakama zashauriwa kutoa nakala za hukumu kwa wakati

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya, imeshauriwa kusimamia na kuhakikisha mahakama za ngazi zote zinatoa kwa wakati nakala za hukumu baada ya kesi kukamilika ili kupunguza malalamiko ya wananchi kuhusu huduma zinazotolewa na mahakama hizo.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, wakati wa uzinduzi wa Wiki ya Sheria ambapo alisema amekuwa akipokea malalamiko ya mara kwa mara kuhusu ucheleweshaji wa nakala hasa kwenye mahakama za ardhi.

Alisema kutokana na malalamiko anayoyapokea kutoka kwa wananchi amekuwa akiziandikia mahakama hizo barua kuzikumbusha kutoa nakala mapema jambo ambalo alisema huwa halileti picha nzuri kwa wananchi.

Homera alisema nakala ya hukumu ya kesi inamsaidia mhusika wa kesi kufanya uamuzi wa hukumu iliyotolewa na mahakama husika, lakini asipoipata anashindwa kufanya uamuzi na wakati mwingine kumfanya akose haki yake.

Alisema mhusika baada ya kupokea nakala ya hukumu anaweza akaamua kuitumia kukata rufani kwenye mahakama ya ngazi inayofuata ama akaamua kuridhika na uamuzi uliofanywa na mahakama husika.

"Kwa mtazamo wangu mambo mengine yote mahakama mnaenda vizuri sana, rekebisheni hiyo kasoro ya kuchelewesha nakala za hukumu hii ndiyo iliyobaki, haipendezi wananchi wawe wanalalamikia kitu kidogo kama hicho," alisema Homera.

Naibu Msajili Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya, Projestus Kahyoza, alisema mahakama hiyo itaufanyia kazi ushauri wa Mkuu wa Mkoa kwa haki kwa kuwa ushauri huo ni kwa ajili ya kuboresha utendaji wa mahakama. Alisema hukumu ni jambo muhimu wakati wa utoaji wa haki kwa wananchi kutokana na kuonyesha mwelekeo wa utoaji wa haki.

Alimshukuru Homera kwa ushauri huo na utekelezaji wa jambo hilo unaanza mara moja kwa kuhakikisha mahakama za ngazi zote zinapewa utaratibu wa namna ya kutekeleza jambo hilo la kisheria.

"Tunashukuru sana kwa kutukumbusha jambo hili muhimu, tutachelewa mambo mengine, lakini sio kwenye suala la hukumu na nikuhakikishie kwamba utekelezaji wa jambo hili unaanza sasa hivi," alisema Kahyoza.

Kwa upande wake, Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya, Rose Ibrahim, alisema katika wiki ya sheria mahakama hiyo itatoa huduma mbalimbali kwa wananchi kuhusu masuala ya kisheria yanayowakabili.

Aliwataka wananchi kujitokeza katika viwanja vya Kabwe jijini Mbeya na huduma hizo zitakuwa zinatolewa bure na wataalamu mbalimbali wa masuala ya kisheria. Alisema katika eneo hilo mahakama hiyo kwa kushirikiana na wadau wake watakuwa wanatoa huduma ya kuwaelimisha wananchi kuhusu ufunguaji wa mashauri na uendeshaji hasa yanayohusiana na ndoa na talaka.

Vilevile, alisema mahakama hiyo itakuwa inatoa elimu kuhusu uendeshaji wa mashauri ya mirathi, ukaziaji wa hukumu na mambo mengine ya kisheria ambayo wananchi watataka wasaidiwe.





## Mufti ataka taratibu za ndoa zizingatiwe

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JAMII imeshauriwa kuzingatia na kuzifuata taratibu za ndoa ili kupunguza migogoro inayojitokeza katika jamii.

Ushauri huo ulitolewa na Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kabi, katika hafla ya ufungaji wa mafunzo ya ndoa iliyofanyika Mjini Zanzibar.

Alisema endapo wanajamii watakamilisha sharti, taratibu pamoja na kupatiwa elimu ya ndoa itasaidia kwa kiasi kikubwa katika kupunguza vitendo viovu ikiwamo udhalilishaji pamoja na migogoro kwa wanandoa.

Alisema kuwa wanajamii wanapaswa kuwalea watoto wao katika misingi ya maadili kwa kuwasomesha elimu ya dini na dunia ili kupata kizazi chenye maadili mema na hatimaye kuleta amani nchini.

Aliwaasa wahitimu wa mafunzo hayo, kwa kuwataka kuyatumia vyema mafunzo waliopatiwa kwa kutekeleza haki na wajibu katika ndoa ili kuishi vizuri katika ndoa zao. Katibu wa Mufti Zanzibar, Sheikh Khalid Ali Mfaume, aliwataka wahitimu hao kuyazingatia vyema mafunzo ya ndoa ili kila mmoja kupata haki yake katika ndoa, kwa lengo la kupunguza migogoro ya ndoa.

Akisoma risala ya wanafunzi wahitimu wa mafunzo ya ndoa, Huwaida Mzee, alisema mafunzo hayo yamewajengea uwezo mkubwa wa kudumisha ndoa pamoja na kuzikabili changamoto katika ndoa.

Aidha, aliahidi kuyazingatia na kuyafanyia kazi mafunzo hayo kwa lengo la kuepusha ongezeko la talaka katika jamii.

Waliiomba ofisi ya Mufti Zanzibar kutunga kitabu maalumu cha maadili ya ndoa ili kuielimisha jamii kwa njia mbalimbali, pamoja na kuiomba serikali kuweka msisitizo kwa wanajamii kupatiwa mafunzo ya ndoa kabla ya kufunga ndoa kwa lengo la kupunguza udhalilishaji nchini.

Jumla ya wahitimu 199 wamehitimu mafunzo ya ndoa awamu ya 12 wakiwamo wanaume 76 na wanawake 123.

# Rais Mwinyi kufungua kongamano la bima Afrika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, anatarajiwa kufungua kongamano la bima la Afrika ambalo litafanyika kesho.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake Kilimani Mjini Zanzibar, Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania, (TIRA), Khadija Said, alisema kongamano hilo litafanyika Zanzibar.

Alisema ujumbe wa kongamano hilo ni ongezeko la ukuaji wa huduma za bima Afrika na kongamano hilo litahudhuriwa na washiriki kutoka nchi za Afrika.

Alisema pia kongamano hilo litashirikisha kampuni 131 za bima Tanzania na mada mbalimbali zitawasilishwa.

"Huduma za bima huwa zinategemeana kutoka kampuni moja kwenda kampuni nyingine kwa sababu dhima ya bima ni kubwa na inatofautiana kati ya daraja na daraja mfano kuna bima za magari, nyumba, moto, meli, ndege, afya," alisema.

Alisema kongamano hilo litasaidia kuyajengea uwezo mashirika ya bima na taasisi binafsi, na kwamba zaidi ya washiriki 300 watahudhuria katika kongamano hilo kutoka nchi za Afrika.

Alisema kwa Zanzibar ni mara ya kwanza kufanyika ambapo kongamano kama hilo kwa mara ya mwisho lilifanyika Zambia mwaka 2019/2020.

Aidha, alisema matumizi ya huduma za bima Tnazania ni asilimia 15 na wanatarajia ongezeko hilo kufikia asilimia 50 ifikapo mwaka 2030 kwa mujibu wa mpango kazi wa taifa. Alisema ufahamu wa bima kwa Watanzania hivi sasa ni asilimia 36, lakini ifikapo mwaka 2030 wanatarajia ufahamu huo kuongezeka hadi asilimia 80.

Naibu kamishna huyo alisema kuwa TIRA itahakikisha inaendelea kuyachukulia hatua za kisheria taasisi zinazotoa huduma za bima ambazo hazifuati sheria ikiwamo kupewa adhabu ya kufungiwa kutoa huduma au kutozwa faini.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya Salum, akizungumza na wavuvi wa Msuka Pemba alipofanya ziara na Kamati ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia ofisi ya viongozi wakuu wa kitaifa walipokuwa wakikagua ukuta wa kuzuia maji ya bahari unaozuia mmomonyoko wa fukwe. **PICHA: RAHMA SULEIMANI**

# Sababu bei ya vifaa vya ujenzi kupaa hii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shabani, ameeleza sababu ya kupanda kwa bei za bidhaa za vifaa vya ujenzi.

Akizungumza na Nipashe kuhusu kupanda kwa bei za bidhaa za vifaa vya ujenzi, waziri huyo alisema sheria ya ushindani halali na kumlinda mlaji Zanzibar, kuna bidhaa ambazo zimetajwa katika sheria na serikali huziwekea bei elekezi.

Alisema bidhaa hizo ni unga wa ngano, mchele, sukari na mafuta ya kula, lakini bidhaa zingine zikiwamo vifaa vya ujenzi inampa mamlaka waziri wa biashara kushughulikia pale ambapo kunaonekana bidhaa kupanda kwa kasi kubwa bila ya sababu za msingi.

Alisema bidhaa za vifaa vya ujenzi kupanda bei kunatokana na changamoto kubwa ya biashara duniani kulikosababishwa na janga la ugonjwa wa UVIKO-19.

Alisema bidhaa za vifaa vya ujenzi hazizalishwi nchini, hivyo nchi zinazozalisha bidhaa hizo viwanda vilifungwa na uzalishaji kusimama kutokana na UVIKO-19, hivyo upatikanaji wake ukawa mgumu.

Alisema baada ya kuja kwa chanjo za UVIKO-19 uchumi wa nchi hizo ulifunguka, lakini changamoto ikawa ya usafirishaji wa bidhaa.

"Baada ya uwapo wa chanjo ya corona wafanyabiashara wakawa wanasafiri kwenda kununua bidhaa, lakini changamoto ikawa usafirishaji wa bidhaa kwa sababu kupata meli ikawa changamoto baada ya uchumi kufunguka bei za usafirishaji zikapanda na safari za meli kuleta bidhaa nchini zikawa chache,"alisema.

Alieleza kuwa biashara ya meli ni kama biashara ya daladala inafuata ruti (njia) ambayo inapaleka mzigo na kuondoka na mzigo.

Alisema kwa mujibu wa sheria ya ushindani halali na kumlinda mlaji, wana dhima ya kuwalinda wafanyabiashara na kuwalinda walaji, hivyo kushusha bei za bidhaa wakati mfanyabiashara katumia gharama kubwa kusafirisha bidhaa ni kumkandamiza mfanyabiashara.

Alisema kupanda na kushuka kwa bidhaa katika biashara hutokea, hivyo wizara hufuatilia bei za bidhaa lengo ni kumlinda mlaji ili bidhaa kupatikana kwa bei nafuu.

Alisema sekta ya biashara inakumbana na changamoto ya milipuko ya kidunia, hivyo hupelekea uzalishaji wa viwanda kusimama na uwekezaji kudorora.

Nipashe ilitembelea baadhi ya maduka ya vifaa vya ujenzi na kukuta bei za vifaa hivyo imepanda, hali ambayo imeibua manung'uniko kutoka kwa wananchi.

**BEI ZA BAADHI YA VIFAA**

Kiroba kimoja cha saruji ya Tanzania ni Sh. 16,000 wakati kabla ya corona iliuzwa Sh. 12,000, saruji ya Oman inauzwa Sh. 18,000 kabla ya corona iliuzwa Sh 14,000 na saruji kutoka Kenya kwa inauzwa Sh. 17,000 kabla ya corona haikuwa sokoni.

Kwa upande wa bei za nondo ya milimita nane inauzwa Sh. 16,000 kabla ya corona ikiuzwa Sh. 8,000, nondo milimita 10 inauzwa Sh. 28,000 kabla iliuzwa Sh. 12,000 na nondo ya milimita 12 inauzwa Sh. 34,000 kutoka Sh. 18,000.

Bati la kawaida kutoka China lenye urefu wa futi 10 linauzwa Sh. 24,000 kutoka Sh. 12,000 na bati maarufu ya Msauzi futi 12 inauzwa Sh. 28,000 kutoka Sh. 18000.

Baadhi ya wananchi waliozungumza na Nipashe, walisema kupanda kwa bei ya bidhaa vya ujenzi ni changamoto kubwa kwao kuendelea na ujenzi wa nyumba za makazi.

"Hapa ninapoishi nimekodi, nataka nimalize nyumba yangu ninayojenga ili nihamie kwangu niondokane na kodi ya nyumba, lakini nashindwa maana ujenzi wenyewe ni wa kinyonge na vifaa vyote vya ujenzi vimepanda bei, hilo bati ndio halisemeki," alisema Ali Issa mkazi wa Kisauni Zanzibar.

Aliiomba serikali kufanya marekebisho ya sheria ili vifaa vya ujenzi kuweka bei elekezi, hali ambayo itasaidia kutopanda kwa bei kiholela kama ilivyo kwa bidhaa zingine.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI
INDUSTR IAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NICHOLAS H MBWANJI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA LAND CRUISER PRADO** yenye namba za usajili **T 802 AJU** chasis namba **LJ950006315,** engine namba **3L4608464,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochiote cha polisi
Polisi taarifa CONTROL NAMBA **9910830255902**

116664102

---

**IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**TEMEKA HIGH COURT SUB-REGISTRY**
**[ONE STOP JUDICIAL CENTRE]**
**AT TEMEKE**
**MATRIMONIAL CAUSE NO.09 OF 2022**

**MERGITU EBBA…………..PETITIONER**
**VERSUS**
**JULIUS MUHUZA……..RESPONDENT**

**NOTICE OF DATE OF HEARING**
**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for hearing on 26th day of January, 2022 at 9:00 am before Hon **MUGETA** judge.

You are required to appear in this court without a failure and you must produce to that day all the documents upon which you intended to reply in support of your case.

**GIVEN** under my hand and seal of the court this 24th day of January, 2022

AG DEPUTY REGISTRAR

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOSEPH BURTON LWANGILI** anatangaza kupotelewa na cheti cha Chuo chenye namba **467/CMLS/T/2013** kilichotolewa na **RUAHA CATHOLIC UNIVERSITY** mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MKB/RB/78/2022.**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**MDENYULUPEMBE PERCIVAL MLOWE anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S4227-0073 kilichotolewa na Baraza na Mitihani la Taifa kupitia LYAMKENA SEKONDARI mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: SIM/MAS/RB/32110/2022.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**VENNY CONSTRUCTION & REAL ESTATE COMPANY LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari aina ya SCANIA namba za usajili **T 904 BUU.** Chassis No. **04484645,** Engine **No.6150430.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi **DOD/DOD/RB/22887/2022.**

116664802

---

**1FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.57 OF 2022**
**In the matter of the Estate of the late PETER PANTALEO MELLA**
**and**
**In the matter of application for letters of administration by**
**PAULINE PETRER MELLA**
**GENERAL CITATION**
**[rule 75]**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate [ or letters of administration] is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 14th day of march 2022

**Dated at DAR ES SALAAM this 21st day of January 2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe mkini**
**Mkoa Njombe**
**Usimamizi wa mirathi na10/2022**
**katika shauri la mirathi ya**
**EDWIN LEONARD KIGODA marehemu wa NJOMBE**
**katika shauri la maombi ya kumteau msimamizi yaliyoletwa na**
**ROSE WILLIAM MHINA mwombaji**

**TANGAZO KWA UMMA**
**[kanuni ya 5[2] ya kanuni za usimamizi wa mirathimahakam za mwanzo]**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 21 mwezi 02 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa kabla au mpaka tarehe tajwa hapo juu.
Zingatia; endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
**Imetolewa leo tarehe 21 mwezi 1 mwaka 2022**

---

**DEED POLL**
**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**
**(CAP.117)**

BY THIS DEED.I undersigned MWAJUMA WAMBURA LUBALE of TELL.NO 0762752550. Do hereby absolutely, renounce and abandon the use of my former name of MWAJUMA WAMBULYALILA NYAMULA and in lieu thereof do assume from the date hereof the name of MWAJUMA WAMBURA LUBALE.
I hereby authorize and request all persons to designate, describe and address me by such assumed name of MWAJUMA WAMBURA LUBALE
In witness whereof, I have hereunder signed my assumed named of MWAJUMA WAMBURA LUBALE in lieu of the relinquished name of MWAJUMA WAMBULYALILA NYAMULA.

**SIGNED and DELIVERED by the said MWAJUMA WAMBURA LUBALE Who is known to me by……………………………………..**

**The latter being known to me in my presence This 10th day of November,2021**

**DEPONENT**

……………………………..
**Before me E.S. MISSANA**
**Signature…………………………**
**Qualification: RESIDENT MAGISTRATE**
**Address: P.O.BOX 10, MASWA**

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe Mjini**
**Mkoa Njombe**
**Usimamizi wa mirathi Na 6/2022**
**Katika Shauri la mirathi ya OVIN BERNOTH MLELWA Marehemu wa KIBENA**
**Katika Shauri la maombi ya kumteua Msimamizi yaliyoletwa na RITA BERNOTH TANGAZO KWA UMMA**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za USIMIZI WA Mirathi Mahakama ya Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 17 Mwezi 02 Mwaka 2022 kabla muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Mapingamizi yoyote kuhusu Maombi haya yawe yameandikishwa kabla au mpaka tarehe tajwa hapo juu.
Zingatia; Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mhakamani kukaguliwa.

**Imetolewa leo tarehe 17 Mwezi 01 Mwaka 2022**

……………………………………………………
**HAKIMU MKAZI**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.201 OF 2021**

**In the matter of the estate of the late of the late ABSALOM OBETH MWAKIPUNDA**

**Of Chamwino Urban within Dodoma City**

**AND**

**In the matter of application for letters of administration by HELLEN SARIA MWAKIPUNDA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **25/01/2022**

Dated at Dodoma this **05/01/2022.**

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**FINDU ADAM NDABA**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.361 CLJ.**YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI
**SON/TUN/RB/28493/2022**




**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Serikali yaweka wazi sababu uhaba, kupanda bei ya vinywaji

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imeeleza sababu za uhaba na kupanda bei ya vinywaji baridi ikidai kuwa umetokana na changamoto ya upatikanaji wa malighafi muhimu zinazohitajika katika uzalishaji wa vinywaji hivyo ikiwamo sukari ya viwandani.

Waziri wa Uwekezaji Viwanda na Biashara Dk. Ashatu Kijaji, akitoa maelezo jana kuhusu suala hilo, alisema bidhaa hiyo ambayo ni muhimu kwa uzalishaji wa vinywaji baridi inaagizwa kutoka nje ya nchi, akisema kuwa kwa nchini hakuna kiwanda kinachozalisha malighafi hiyo jambo lililochangia uhaba wake.

Alisema changamoto ya uagizaji wa sukari ya viwandani imechangiwa na upungufu wa makasha ya kusafirishia shehena katika soko la dunia kuokana na athari za UVIKO-19.

"Jambo hili limepatiwa ufumbuzi kwa sasa na sukari imeendelea kuingizwa nchini kwa njia ya ufungashaji usiotumia makasha, katika kipindi cha Desemba na Januari, na kwa kipindi hicho tumeshapokea tani 25,000 za sukari," alisema Ashatu.

Aliongeza kuwa serikali imechukua jitihada hizo kuhakikisha tatizo hilo linakwisha ili wazalishaji wa vinywaji baridi waendelee kuzalisha, na alidai kuwa kwa sasa nchini haina upungufu wa sukari ya viwandani na uzalishaji wa vinywaji baridi unaendelea katika viwanda vyote.

Aidha, alisema uchunguzi wao ulibaini kuwa kupanda kwa bei za vinywaji haukuanzia viwandani ila ilichangiwa na wafanyabiashara na wasambazaji wasio waaminifu, kwani walipandisha bei kinyume na taratibu.

Alisema kutokana na uchunguzi huo, serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa kushirikiana na wazalishaji na wafanyabiashara ili kudhibiti upandaji holela wa bei za vinywaji na bidhaa zinginezo.

"Kama waziri mwenye dhamana, ninazielekeza mamlaka na taasisi mbalimbali za serikali ambazo zimepewa dhamana ya kusimamia mienendo ya masoko ya bidhaa kutekeleza wajibu wao kikamilifu na kwa umakini mkubwa ili kudhibiti upandishaji holela wa bei za bidhaa nchini.

"Hilo lifanyike ili kumlinda mlaji na mzalishaji ambaye hajapandisha bei, lakini katikati wanatokea mawakala wanaopandisha bei na kumuharibia hata mzalishaji kwa hiyo taasisi zetu ziweze kufanya kazi yao vizuri," aliagiza Ashatu.

Pia aliwaelekeza maofisa biashara wa mikoa na wilaya nchini kufuatilia kwa ukaribu mwenendo wa bei za bidhaa mbalimbali katika maeneo yao na kuwasilisha taarifa hizo kila mwezi kupitia ofisi za mkuu wa mikoa ili waweze kuchukua hatua stahiki na kwa wakati pale inapotokea kuwa na utofauti wa bei za sokoni na ambazo wananchi wanalipishwa.

# Mamia washiriki maziko ya familia iliyouawa

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

MAMIA ya watu wakiwamo viongozi wa serikali walijitokeza juzi kushiriki maziko ya watu watano wa familia moja waliouawa na watu wasiojulikana na miili yao kutelekezwa ndani ya nyumba yao katika kijiji cha Zanka wilayani Bahi.

Miili ya watu hao ilizikwa juzi katika kijiji hicho huku Diwani wa Kata hiyo, Deo Jeuza, akiomba serikali kuongeza idadi ya askari ili kukomesha matukio ya mauaji ambayo yamekuwa yakitokea mara kwa mara katika eneo hilo.



Akizungumza na Nipashe diwani huyo alisema katika kata yake tukio hilo si mara ya kwanza kutokea kwani mauaji kama hayo yamekuwa yakitokea mara kwa mara.

"Kata yangu imekuwa na matukio ya mauaji kama haya mengi sana mwaka juzi katika kijiji cha Mkondai waliuawa watu watatu wa familia moja; mama, baba na mtoto walikutwa wamechomwa na vitu vyenye ncha kali na kutelekezwa ndani na hakuna mtu ambaye alikamatwa hadi leo.

"Mwaka ule mwingine pia aliuawa mtu mmoja kwa kukatwa kichwa na kutenganishwa na kiwiliwili chake, juzi tena limetokea hili naiomba serikali kupitia Jeshi letu la Polisi kutusaidia kuongeza doria katika kata yetu,"alisisitiza diwani huyo.

Aidha, alisema anashauri Jeshi la Polisi kutumia ulinzi shirikishi kwa kushirikiana na wananchi wa eneo hilo hili kudumisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao.

Alisema changamoto ya ukubwa wa jiografia ya eneo la kata hiyo kutokuwa rafiki hivyo mtu yeyote anaweza kufanya tukio na kutokomea kusikojulikana bila kufikiwa na vyombo vya ulinzi na usalama.

Akizungumzia tukio la mauaji ya watu watano wa familia amoja, aliwataka wakazi wa kijiji hicho kushirikiana na uongozi wa serikali yao kutoa taarifa za wanaohusika kufanya uhalifu huo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, Donald Mejeti, alisema watahakikisha wahusika wote walihusika na tukio hilo wanakamatwa ili kurejesha imani kwa wananchi.

"Jambo hili sisi kama viongozi limetuchanganya sasa, lakini mambo ambayo tunakwenda kuyafanyia kazi ni kuhahakisha wote walihusika wanakamatwa ili kurejesha imani kwa wananchi, lakini wahalifu kutambua kuwa dola iko," alisema Mejetii.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Onesmo Lyanga (pichani), alipotafutwa kuzungumzia uchunguzi wa tukio hilo umefikia hatua gani, alisema bado wanaendelea na uchunguzi.

# Mrithi Maalim Seif ACT wiki hii

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeitisha mkutano mkuu kwa ajili ya kujaza nafasi za Mwenyekiti wa Chama Taifa, Makamu Mwenyekiti Taifa upande wa Zanzibar na Mjumbe wa Halmashauri Kuu.

Nafasi ya uenyekiti taifa inajazwa kuziba pengo la Hayati Maalim Seif Sharif Hamad, aliyefariki dunia Februari 17, mwaka jana.

Mkutano huo utakaofanyika kuanzia Alhamisi, utahudhuriwa na vyama vikuu vya upinzani katika nchi za Afrika, kikiwamo MDC Alliance cha Zimbabwe, UPND (Zambia), UTM (Malawi), UNC (Congo DRC) ODM (Kenya) na NUP (Uganda).

Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu, akizungumza na waandishi wa habari jana, mkoani Dar es Salaam, alisema mbali na uchaguzi wa viongozi hao, pia utafanyika uzinduzi wa mfumo wa ACT Kiganjani kuongeza kasi ya uendeshaji chama.

Shaibu alisema mgeni rasmi katika uzinduzi wa mfumo wa ACT-Kiganjani na mkutano huo, anatarajiwa kuwa Nelson Chamisa, Rais wa Chama cha MDC Alliance ambacho ni chama kikuu cha upinzani Zimbabwe.

"Chama cha ACT-Wazalendo kitafanya mkutano mkuu maalum na kuzindua mfumo wa kuisimamia na kuiwajibisha serikali. Kamati Kuu ya chama itakaa Jan. 27 na Halmashauri Kuu Januari 28, mwaka huu," alisema Shaibu.

Aliongeza kwamba utafanyika mdahalo wa wagombea wa nafasi za uenyekiti na makamu mwenyekiti taifa na kwamba wahudhuriaji pia na watakuwa wanasiasa mbalimbali kutoka vyama vya upinzani kutoka nchi hizo.


SIMBA CEMENT
STRENGTH WITHIN

## NOTICE TO MEMBERS

**TANGA CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY**

**(Incorporated in the United Republic of Tanzania)**

The twenty seventh Annual General Meeting of Shareholders of Tanga Cement Public Limited Company will be held on Friday 25 February 2022 at 10H30, online through the Microsoft Teams platform (invitations will be sent by email and sms to shareholders) for the following purposes:

**1. Notice of Meeting**
Notice convening the meeting to be taken as read.

**2. Approval of Minutes**
To approve and sign the minutes of the twenty sixth Annual General Meeting held on 27 November 2020.

**3. Financial Statements and Directors' Reports**
To review and adopt the Financial Statements and Directors' report for the year ended 31 December 2020.

**4. Dividend for the year ended 31 December 2020**
Shareholders to note the proposal from the Board not to declare a final dividend for the financial year ended 31 December 2020.

**5. Appointment of Directors**
To appoint Directors to the Board who retired by rotation.

**6. Approval of Directors Remuneration**
To approve the non-executive directors' remuneration for the 2021 financial year.

**7. Appointment of External Auditors**
To approve the appointment of the External Auditors for the 2021 financial year.

**8. General**
Any other business.

Any member entitled to attend and vote at the meeting is entitled to appoint a proxy or proxies to attend and vote on their behalf. If a member is an organisation then such members must submit proxy forms and a Board resolution to approve the appointment of the proxy. These proxies are to reach the registered office of the Company not less than 48 hours before the time of the meeting. Members and holders of proxies are required to bring with them acknowledgements of receipt of delivery of proxy forms, copies of proxy forms and identification card for registration purpose.

**By order of the Board.**

Qurесh Ganijee
**Company Secretary**
25 January 2022

166662

# TANZANITE YAIENDEA ETHIOPIA KARATU

**Na Saada Akida**

TIMU ya Taifa ya Wanawake chini umri wa miaka 20, Tanzanite imekwenda Karatu kwa ajili ya kuweka kambi ya maandalizi ya mchezo wa marudiano wa kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Ethiopia utakaopigwa mapema mwezi ujao. Katika mchezo uliochezwa juzi visiwani Zanzibar, Tanzania ilipata ushindi wa 1-0.

Katibu Mkuu wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Kidao Wilfred alisema anawapongeza wachezaji kupambana na kuzuia wapinzani wao kutopata bao la kusawazisha.

Alisema hatua ya nne ni ngumu na ushindani mkubwa na kuelekea mchezo wa ugenini wanalazimika kwenda kuweka kambi Karatu kwa ajili ya kuzoea mazingira ya hali ya hewa.

"Tuna wapongeza wachezaji wetu kupambana na kuweza kuwazuia wapinzani wetu kupata bao la ugenini, hii hatua ni ngumu sana," alisema.

> **"Ethiopia sio wa kuwa beza kwa sababu kabla ya hatua hii waliwafunga Botswana, hii unaona ugumu wa wapinzani wetu, tuna imani Karatu kuna mazingira mazuri ya maandalizi ya timu yetu."**

Naye Kocha Mkuu wa Tanzanite, Bakari Shime, alisema timu inaenda Karatu kwa ajili ya hali ya hewa ambayo inafanana na Ethiopia licha ya kutofautiana kwa asilimia tano.

Alisema baada ya ushindi wa nyumbani wana wakati mgumu sana mchezo wa maruadiano kwa sababu watakuwa ugenini.

"Tuko katika hatua ngumu sana, hii michezo ni migumu sana na tunatafuta mbinu ya kuwatoa nyumbani kwao, aina ya uchezaji wa Ethiopia wanapita kati kati ya kiwanja, mechi ijayo watafunguka na kushambulia," alisema Shime.

Alisema watakuwa makini kufanyia kazi mapungufu yao na ubora wa Ethiopia, kwa sababu tunahitaji kupata uwiano mzuri katika safu yetu ya ushambuliaji na ulinzi.




Wasanii wa kikundi cha Mnaa Theatre Mabibo Dar es Salaam, wakiimba mashairi katika mkutano wa kuwajengea uwezo wadau wa mapambano dhidi ya rushwa ya ngono kwa wanafunzi mwishoni mwa wiki iliyopita. Mkutano huo uliandaliwa na Shirika la Wanawake katika jitihada za kimaendeleo (WAJIKI). **PICHA: SABATO KASIKA**

# *Julio: Coastal wanacheza kitoto*

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuichapa Coastal Union juzi jioni kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga mabao 3-1, Kocha Msaidizi wa Namungo, Jamhuri Kihwelo 'Julio' amesema wapinzani wao si timu mbaya ila wachezaji wake wanacheza kitoto sana ili kuwaonyesha mashabiki kuwa wanaweza, hivyo kushindwa kucheza kwa malengo ya kutafuta ushindi.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, Julio alisema kuwa pia klabu hivyo bado inaathiriwa kisaikolojia na kupoteza mechi iliyopita dhidi ya Yanga, ambako kulizuka mgogoro unaowaathiri pia wachezaji wao.

Namungo iliichapa Coastal Union mabao 3-1 yaliyowekwa wavuni na Reliatns Lusajo akifunga mabao mawili na Obrey Chirwa moja, huku bao la kufutia machozi la wenyeji likiwekwa ndani ya nyavu na Haji Ugando.

"Kupata mabao matatu hasa ukiwa ugenini si jambo dogo, tunashukuru vijana wetu wamefuata maelekezo hasa kipindi cha pili ambapo tulicheza vizuri sana. Coastal wanacheza vizuri, lakini wanacheza kitoto sana, wanataka watu majukwaani wawaone kama wanaweza kucheza mpira badala ya kucheza soka la malengo kutafuta matokeo. Pia inaonekana tangu walipofungwa na Yanga hawajakaa sawa. Kuna migongano imetokea ambayo inaonekana imewaathiri hata wachezaji wao," alisema Julio, mchezaji na kocha wa zamani wa klabu ya Simba.

Kocha Msaidizi wa Coastal Union, Shaaban Bakari, amesema kuwa makocha wa safu ya ulinzi wamesababisha wapinzani wao kupata mabao hayo.

"Siamini kama presha ya mashabiki nje, imesababisha kufungwa, ila ni makosa ya kimchezo yaliyotufanya tupoteze," alisema.

Kwa matokeo hayo, Coastal Union imekaa kwenye nafasi ya saba ikiwa na pointi 17, huku Namungo ikiwa ya sita kwa pointi 17, zikitofautiana mabao ya kufunga na kufungwa.

## Lusajo amwacha Mayele kwenye kona

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili aliyoyafunga straika wa Namungo Reliants Lusajo kwenye mechi ya juzi dhidi ya Coastal Union, yamemfanya machezaji huyo kufikisha mabao saba na kumpita Fiston Mayele wa Yanga ambaye amesalia na mabao sita kwenye mbio za kuwania kiatu cha dhahabu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga, Lusajo alipachika mabao mawili ndani ya dakika tatu, akiipa timu yake ya Namungo ushindi wa ugenini wa mabao 3-1 dhidi ya Coastal Union.

Ilikuwa ni kwenye dakika ya 85 na 87, straika huyo aliyekuwa na mabao matano, akafikisha mabao saba.

Kwa sasa Lusajo anasimama kama kinara wa mabao kwenye Ligi Kuu akiwa na idadi hiyo ya mabao, huku Mayele, straika raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo akiwa na mabao sita akishika nafasi ya pili.

Straika huyo pamoja na kufanya kazi kubwa juzi kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha ya kukokota mpira kwa umbali mrefu na kutoa pasi ya mwisho ya bao pekee kwenye mechi hiyo dhidi ya Polisi Tanzania, alishindwa kupata bao na kusalia na idadi hiyo ya mabao.

Wachezaji wanaofuata baada ya hao ni wenye mabao matano, nao ni Vitalis Mayanga wa Polisi Tanzania, George Mpole wa Geita Gold, Jeremiah Juma na Prisons.

Wenye mabao manne ni Richardson Ng'ondya na Juma Luzio wa Mbeya City, Mateo Antony wa KMC, Feisal Salum wa Yanga na Meddie Kagere wa Simba.

## 'Kibonge Mwepec' kurejea upya

**Na Sabato Kasika**

BAADA ya kimya zaidi ya miaka miwili, rapa Witnez 'Kibonge Mwepec' amesema sasa anajiandaa kurejea upya kwenye 'gemu' ili kuendeleza muziki wa Hip Hop, huku akiwa na nyimbo nane mpya kibindoni.

Akizungumza na gazeti hili jana, msanii huyo amesema, alikaa kimya kwa muda huo kutokana na tatizo la kiafya, na kwamba hali yake inaendelea kuimarika na kwamba anajipanga kushuti video ya nyimbo zake.

"Mashabiki wangu wamekosa kazi zangu, lakini niwaambie kuwa afya yangu inaendelea vizuri baada ya kusumbuliwa kwa miaka mitatu, na niko mbioni kurudi kwenye gemu nikiwa na nyimbo mpya nane," amesema Kibonge Mwepec.

Msanii huyo hakutaja majina ya nyimbo zake, kwa madai kwamba kufanya hivyo kunaweza kusababisha wajanja wakayachukua majina hayo ya kwenda kutumia katika nyimbo zao.

"Jambo la msingi ni kwamba, afya yangu tayari imeimarika na nijiandaa kurudi kuimba Hipo Hop nikiwa na nyimbo nane mpya ambazo wiki chache zijazo nitaanza kurekodi na kushuti video zake," amesema.

Kibonge Mwepec ni miongoni mwa marapa wachache wa kike ambao wamejipatia umaarufu kwenye muziki huo kutokana na jinsi anavyojiamini na kutikisa mwili wake mnene.

Mbali na kuwa rapa, msanii amewahi kushirikishwa katika mashindano mbalimbali yakiwamo ya Bongo Star Search (BSS) kama mmoja wa majaji wa kusaidia kuibua vipaji vya muziki wa kizazi kipya..

## ZISIKUPITE

### ARSENAL WAKWAMA

MPANGO wa Arsenal kumnunua mshambuliaji Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 21, umekuwa mgumu zaidi baada ya Juventus kumletea mmiliki wa Fiorentina, Rocco Commisso ofa pinzani kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Serbia. (**Times**)

### CAMAVINGA ATAKIWA LIVER

LIVERPOOL wanamfuatilia, Eduardo Camavinga kutoka Real Madrid kwa kuwa wamekuwa wakivutiwa na kiungo huyo wa kati wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 19. (**El Nacional**)

### LINGARD MAMBO BADO

KIUNGO wa kati wa England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 29, anatafuta uhamisho wa mkopo kutoka Manchester United katika dirisha la Januari, lakini yuko tayari kumaliza mkataba wake hapo Old Trafford. (**Manchester Evening News**)

### NYOTA KUONDOKA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur, ipo tayari kumuuza mchezaji wa England, Dele Alli na mchezaji wa kimataifa wa Argentina, Giovani Lo Celso, wote wenye umri wa miaka 25, baada ya wachezaji hao wawili kuachwa nje ya kikosi cha Antonio Conte kwa mchezo dhidi ya Chelsea Jumapili. (**Goal**)

### SPURS YAMTAKA TANNER

TOTTENHAM Hotspurs imefanya mpango wa kutaka kumsajili winga, Ollie Tanner mchezaji anayecheza katika timu ambayo haiko katika madaraja rasmi ya soka, Brighton nao wanamwinda nyota huyu. (**Athletic - subscription required**)

### ERIKSEN KUTUA BRENTFORD

KLABU ya Brentford inakaribia kukamilisha masharti ya mkataba wa miezi sita na kiungo wa kati wa Denmark, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 29. (**Sky Sports**)

### BAKKER HUYO NEWCASTLE

NEWCASTLE United inakaribia kumsajili mlinzi wa kushoto wa Uholanzi, Mitchel Bakker mwenye umri wa miaka 25, kutoka Bayer Leverkusen.(**Mirror**)

### MELO SAFI ARSENAL

ARSENAL wamekubali makubaliano ya mkataba wa mkopo hadi mwisho wa msimu wa kiungo wa kati wa Juventus na Brazil, Arthur Melo, 25. (90min).

### LIVERPOOL INAMTAKA CARVALHO

LIVERPOOL inamfuatilia winga wa Fulham mwenye umri wa miaka 19 na timu ya taifa ya England, Fabio Carvalho. (**Fabrizio Romano**)

### ZAPATA ANUKIA NEWCATLE

MATUMAINI ya Newcastle ya kumsajili mshambuliaji wa Atalanta, Duvan Zapata yameongezewa nguvu kutokana na nia ya timu hiyo ya Serie A kumtoa kwa mkopo nyota huyo wa kimataifa wa Colombia mwenye umri wa miaka 30. (**Kioo kupitia HITC**).

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RANGNICK: WASIO NA UWEZO KUONDOKA MANCHESTER UTD

**●●● Athibitisha kuwa mastaa kibao watauzwa au kutolewa kwa mkopo kwa sababu...**

**MANCHESTER,** Uingereza

KLABU ya Manchester United iko kwenye mazungumzo na klabu pinzani katika harakati za kutafuta suluhu kwa nyota wao wanaotaka kuondoka, kwa mujibu wa kocha wa muda, Ralf Rangnick.

Kuna idadi ya wachezaji wa hadhi ya juu kwenye viunga vya kikosi cha United kilichojumuishwa kwa gharama kubwa ambao wanaweza kutaka kuhama kabla ya dirisha la usajili la Januari kufungwa.

Ripoti zinaonyesha Jesse Lingard, Anthony Martial na Donny van de Beek ni miongoni mwa wale ambao wanaweza kutarajia kuondoka kabla ya mwisho wa mwezi huu.

**Lingard analengwa na Newcastle United, Rang nick alifichua kabla ya ushindi wa Jumamosi dhidi ya West Ham , wakati Sevilla wanadai wa kumtaka Martial.**

Hapo awali ilipendekezwa kuwa Mashetani Wekundu hao wangesita kupunguza ukubwa wa kikosi chao kutokana na hatari ya kuachwa pungufu iwapo kutatokea mlipuko wa virusi vya corona.

Lakini maoni ya hivi karibuni ya Rangnick yanaonekana kuashiria United ipo tayari kuwaachia wachezaji hao ambao wanaona mustakabali wao kwingineko.

"Sijui (nini kitakachotokea)," alisema kocha huyo. "Najua ni wachezaji gani wangetaka kuondoka.

"Najua kuna mazungumzo na klabu, lakini sihusiki katika hilo. Labda nitatumwa na kufahamishwa kama kuna kitu kinatokea. Sote itabidi tusubiri na kuona kitakachotokea."

LIVE IN PLAY | CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 878

MECHI KALI
SENEGAL
VERSUS
CAPE VERDE
1 | 1.64
X | 3.41
2 | 5.94

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# RAMOS AKUNWA NA BAO LAKE LA KWANZA

**PARIS,** Ufaransa

SERGIO Ramos anatumaini bao lake la kwanza pale Paris Saint-Germain litakuwa moja ya mabao mengi baada ya kufungua akaunti yake kwa klabu hiyo.

Beki huyo alifunga bao hilo katika kipindi cha pili katika uwanja wa Parc des Princes wakati PSG wakipata ushindi mnono wa 4-0 dhidi ya Reims.


Ramos alianza kwa mara ya pili kwenye kikosi cha PSG baada ya kuwa nje kwa muda mrefu kutokana na kusumbuliwa na majeraha tangu alipotua hapo akitokea Real Madrid.

"Nina furaha sana kwa ushindi huu na kwa bao langu la kwanza na timu hii," alisema Ramos akiiambia Amazon Prime Video. "Nimefurahi nilicheza kwa dakika 90. Ninapenda kuungwa mkono na mashabiki. Ni vizuri kuchukua pointi tatu.

"Hili ni bao langu la kwanza na PSG na ninatumaini kutakuwa na mengi zaidi. Jambo muhimu ni kuimarika kimwili siku baada ya siku."

Mauricio Pochettino, ambaye timu yake iliendeleza ushindi nyumbani naye alionyesha furaha yake kwa Ramos.

"Nina furaha kwa ajili yake. Ni muhimu kwake kumaliza mchezo," alisema Pochettino.



## Chiesa kuukosa msimu mzima

**TURIN,** Italia

WINGA wa Juventus, Federico Chiesa hatacheza tena msimu huu baada ya kufanyiwa upasuaji wa goti Jumapili.

Miamba hao wa Serie A walisema Chiesa huenda akakaa nje kwa takriban miezi saba, kumaanisha kwamba anaweza kurejea katika hatua za awali za msimu wa 2022-23.

Hiyo inamaanisha kuwa Chiesa ataondolewa katika mipango ya Italia ya mechi ya mchujo wa kufuzu Kombe la Dunia.

Mabingwa hao wa Ulaya watamenyana na Macedonia Kaskazini katika nusu-fainali ya mchujo Machi na kisha watakutana na Uturuki au Ureno kuwania kufuzu kwenda Qatar.

Chiesa aliumia katik ushindi wa 4-3 wa Seri A dhidi ya Roma ya Jos Mourinho wiki mbili zi lizopita.

Klabu hiyo ilisema kati ka taarifa Jumapili: "Mcha na wa leo (juzi), Federic Chiesa alifanyiwa upasua ji wa goti lake la kushot na atakuwa nje kwa muda wa miezi saba."

,152,880

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 29/01/22 | 18:00 | Amorebieta vs Girona | 2.80 | 3.09 | 2.50 |
| 02. 29/01/22 | 18:00 | Tranmere vs Forest Green | 2.64 | 3.18 | 2.59 |
| 03. 29/01/22 | 18:00 | Oldham vs Rochdale | 2.80 | 3.25 | 2.41 |
| 04. 29/01/22 | 18:15 | Nancy vs Amiens | 2.52 | 3.16 | 2.77 |
| 05. 29/01/22 | 23:00 | Real Oviedo vs Almeria | 2.75 | 3.09 | 2.55 |
| 06. 29/01/22 | 23:00 | SBV Excelsior vs Emmen | 2.56 | 3.49 | 2.46 |
| 07. 30/01/22 | 16:30 | Vicenza vs Alessandria | 2.66 | 3.05 | 2.66 |
| 08. 30/01/22 | 18:30 | FC Sion vs Grasshoppers | 2.56 | 3.40 | 2.56 |
| 09. 30/01/22 | 18:30 | FC Vizela vs Vitoria Guimaraes | 2.90 | 3.20 | 2.47 |
| 10. 30/01/22 | 19:00 | Cardiff vs Nottingham | 2.55 | 3.20 | 2.80 |
| 11. 30/01/22 | 20:30 | PAOK vs Olympiakos | 2.61 | 3.10 | 2.71 |
| 12. 30/01/22 | 23:00 | Lens vs Monaco | 2.77 | 3.26 | 2.46 |
| 13. 30/01/22 | 23:00 | Ponferradina vs Tenerife | 2.42 | 3.11 | 2.91 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 25/01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 19:00 | 4359 | Senegal vs Cape Verde | 1.64 | 3.41 | 5.94 |
| 20:45 | 3048 | Royal Antwerp vs St Truiden | 1.70 | 3.81 | 4.45 |
| 22:00 | 1839 | Hartlepool vs Charlton | 2.69 | 3.31 | 2.34 |
| 22:00 | 3211 | Morocco vs Malawi | 1.29 | 4.55 | 12.85 |
| 22:00 | 3509 | Rotherham vs Cambridge Utd | 1.33 | 4.72 | 7.33 |
| 22:00 | 5354 | SBV Excelsior vs ADO Den Haag | 2.33 | 3.43 | 2.74 |
| 22:45 | 1195 | Luton Town vs Bristol City | 1.78 | 3.48 | 4.31 |
| 22:45 | 1410 | Walsall vs Bradford City | 2.45 | 3.30 | 2.71 |
| 22:45 | 1460 | Lewes vs Cray Wanderers | 1.45 | 4.63 | 5.20 |
| 22:45 | 1551 | Fleetwood Town vs Plymouth | 3.03 | 3.52 | 2.14 |
| 22:45 | 1617 | Braintree vs Welling | 1.97 | 3.66 | 3.13 |
| 22:45 | 1961 | Torquay vs Solihull Moors | 2.09 | 3.33 | 3.28 |
| 22:45 | 2037 | Dartford vs Concord Rangers | 1.47 | 4.25 | 5.42 |
| 22:45 | 2565 | Clyde vs Airdrieonians | 3.27 | 3.46 | 2.04 |
| 22:45 | 2594 | Glenavon vs Dungannon Swifts | 1.42 | 4.90 | 6.60 |
| 22:45 | 2625 | Bromley vs Woking | 1.87 | 3.62 | 3.67 |
| 22:45 | 2695 | Scunthorpe vs Bristol Rovers | 2.80 | 3.29 | 2.39 |
| 22:45 | 2883 | Flint Town United vs Gap Connahs Quay | 3.18 | 3.42 | 2.03 |
| 22:45 | 2964 | Dover vs Eastleigh | 5.65 | 4.29 | 1.48 |
| 22:45 | 3025 | Cliftonville Belfast vs Linfield Belfast | 2.89 | 3.13 | 2.30 |
| 22:45 | 3196 | Carrick Rangers vs Ballymena Utd | 2.64 | 3.51 | 2.29 |
| 22:45 | 3222 | Weymouth vs Dagenham and Redbridge | 3.92 | 3.72 | 1.78 |
| 22:45 | 3305 | Glentoran Belfast vs Coleraine FC | 1.55 | 3.94 | 5.00 |
| 22:45 | 3337 | St Mirren vs Aberdeen | 3.06 | 3.06 | 2.37 |
| 22:45 | 3771 | Burton vs MK Dons | 2.71 | 3.35 | 2.42 |
| 22:45 | 3804 | AFC Wimbledon vs Ipswich | 2.93 | 3.37 | 2.26 |
| 22:45 | 3974 | Portadown FC vs Crusaders Belfast | 6.16 | 4.52 | 1.40 |
| 22:45 | 3985 | Gillingham vs Shrewsbury | 3.00 | 3.29 | 2.26 |
| 22:45 | 4045 | Stockport vs Maidenhead U | 1.23 | 5.65 | 10.72 |
| 22:45 | 4049 | Nottingham vs Barnsley | 1.72 | 3.49 | 4.72 |
| 22:45 | 4269 | Chorley vs AFC Fylde | 2.33 | 3.33 | 2.70 |
| 22:45 | 4486 | Birmingham vs Peterborough | 1.86 | 3.39 | 4.02 |
| 22:45 | 4579 | QPR vs Swansea | 2.08 | 3.30 | 3.39 |
| 22:45 | 4598 | Wealdstone vs Notts County | 3.47 | 3.52 | 1.95 |
| 22:45 | 4626 | Coventry vs Stoke City | 2.29 | 3.18 | 3.04 |
| 22:45 | 4627 | Cardiff Met Uni. vs Barry Town FC | 1.78 | 3.66 | 3.76 |
| 22:45 | 4828 | Chippenham Town vs St.Albans | 2.70 | 3.33 | 2.33 |
| 22:45 | 4857 | Aldershot vs Southend | 2.31 | 3.28 | 2.89 |
| 22:45 | 4901 | Wrexham vs Grimsby | 1.70 | 3.71 | 4.40 |
| 22:45 | 5117 | Boston Utd vs Farsley Celtic | 1.56 | 3.85 | 5.01 |
| 22:45 | 5122 | Benfica vs Boavista | 1.23 | 5.40 | 9.63 |
| 22:45 | 5204 | Elgin City vs Kelty Hearts FC | 4.70 | 4.00 | 1.68 |
| 22:45 | 5292 | Leyton Orient vs Newport | 2.16 | 3.39 | 3.10 |
| 22:45 | 5565 | Hampton and Richmond vs Bath City | 1.78 | 3.62 | 3.82 |
| 22:45 | 5632 | Barrow vs Salford City | 2.50 | 3.24 | 2.70 |
| 22:45 | 5810 | Sutton United vs Harrogate | 2.17 | 3.33 | 2.95 |
| 22:45 | 5923 | Halifax vs Boreham Wood | 2.08 | 3.36 | 3.27 |
| 22:45 | 5977 | Warrenpoint vs Larne | 6.93 | 5.20 | 1.31 |
| 23:00 | 4789 | KAA Gent vs Oostende | 1.31 | 5.13 | 8.48 |
| 23:00 | 5190 | Charleroi vs Kortrijk | 1.90 | 3.60 | 3.70 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# KAGERA SUGAR YAIPIGA MKWARA SIMBA SC

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kesho vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara Simba wakitarajiwa kukabiliana na Kagera Sugar kwenye mchezo wa kiporo, tayari wenyeji hao wameshaanza kuwatisha wapinzani wao kwenye mtandao wa kijamii, ikiwaambia wanachama na mashabiki wa timu hiyo kuwa magari ya kubebea wagonjwa yatakuwapo ya kutosha.

Kwenye mtandao wao wa instagram, Kagera Sugar wameweka baadhi ya video fupi ya mechi kati ya timu hizo mbili.

Mechi hiyo ile iliyochezwa msimu wa 2017/18 ambayo Kagera Sugar ilishinda bao 1-0 kwenye mechi ya mwisho ya Ligi Kuu Tanzania Bara mbele ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati huo, Dk. John Magufuli, aliyekuwa mgeni rasmi.

"Hapa kuna watu walizimia jukwaani baada ya Juma Kaseja kupangusa mkwaju wa penalti ya Emmanuel Okwi, tukutane Jumatano Kaitaba, mtu apigwe tena na kitu kizito kichwani. Magari ya wagonjwa yatakuwapo ya kutosha kutoka hospitali zote za mkoa wa Kagera, kwa hiyo nyie zamieni tu." Ni maneno yaliyoandikwa kwenye mtandao rasmi wa instagram wa klabu ya Kagera Sugar.

Awali mechi hiyo ilipaswa kucheza Desemba 18, mwaka jana, lakini iliahirishwa na Bodi ya Ligi kutokana na wachezaji wengi wa Simba kukutwa na maambukizo ya ugonjwa wa mafua, kukohoa, kichwa na homa kali, hivyo kusababishwa mechi isifanyike kwenye Uwanja wa Kaitaba.

Timu hizo zitakutaka, huku Simba ikiwa imetoka kusuluhu dhidi ya Mtibwa Sugar, ikiwa nafasi ya pili kwa pointi 25, huku Kagera Sugar ikiwa kwenye nafasi ya 11 kwa pointi 13.



Mkurugenzi wa Michezo, Yusuph Singo (wapili kushoto), akimkabidhi kombe la ubingwa wa mashindano ya mbio za magari, Gurpal Sandhi (kushoto), wengine ni viongozi wa Chama cha Mchezo huo nchini (AAT). **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

# *AESL yatamba mbio za magari*

**Na Faustine Feliciane**

MADEREVA wa magari kutoka timu ya AESL juzi wameibuka washindi wa jumla kwenye mbio za magari zilizofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

Gurpal Sandhi na Dave Sihoka waliibuka na ushindi kwenye mbio hizo kwa upande wa NRC2 kwa kujikusanyi alama 169.

Akizungumza wakati wa kuwakabidhi zawadi za ushindi Mkurugenzi wa Maendeleo ya Michezo, Yusuph Singo, alisema kuwa mashindano hayo yameleta tija na kuuinua tena mchezo huo wa mbio za magari.

Aidha, Singo ametoa onyo kwa mtu au taasisi nyingine kutoandaa mashindano kama hayo pasipo kufuata utaratibu na kibali kutoka kwa mamlaka husika.

"Kuhusu Chama cha Mbio za Magari (AAT) kupata eneo, niwaombe wenzangu tuendelee kushirikiana na Baraza la Michezo ambao nao watashirikiana na wizara ili kuangalia namna ya kutatua ombi lenu," alisema Singo.

Kwa upande wake Rais wa AAT, Nizar Jivan, aliwapongeza washindi na wadhamini wote wa mashindano ya mwaka huu, huku akisema janga la corona limeleta changamoto katika kuandaa mashindano hayo.

"Mwaka jana tulishindwa kuandaa mashindano haya kwa sababu ya changamoto ya corona, niwapongeze madereva wote walioshiriki lakini zaidi kwa washindi," alisema Jivan.

Mshindi wa pili kwenye mashindano hayo ni Mandeep Dhani kutoka Team Hari Singh akimaliza na alama 101 na David Matete kutoka timu Amapiano Motorsports akishika nafasi ya tatu kwa kujikusanyia alama 104.

Nafasi ya tatu kwenye mashindano hayo imeshikwa na Manveer Birdi kutoka timu BRT kwa kupata alama 92.

# Michezo

Jumanne Januari 25, 2022

Nipashe




Ramos akunwa na bao lake la kwanza UKURASA 22



Kiungo wa Yanga Feisal Salum 'Feitoto' (katikati), akiwa na wachezaji wa timu hiyo wakishuka kwenye ndege kutoka mkoani Arusha baada ya mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Polisi Tanzania uliopigwa Jumapili. **PICHA: YANGA**

## Simba sc kuivaa Kagera Sugar

**Na Saada Akida**

SIMBA baada ya kukosa bao ndani ya dakika 180 katika michezo miwili ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Pablo Franco, ameendelea kuimarisha safu yake ya ulinzi kuelekea mechi yao dhidi ya Kagera Sugar kesho.

Akizungumza na gazeti hili jana, Pablo alisema wanaendelea na programu yake kuhakikisha wanafanyia kazi mapungufu yao kuelekea mechi yao dhidi ya Kagera Sugar.

Alisema wamejiandaa vizuri kisaikolojia wachezaji wake kukabiliana na mechi za karibu kuhakikisha wanapata matokeo chanya katika mchezo huo.

"Ligi imekuwa ngumu, kila timu imejipanga vizuri na sisi tumefanya maandalizi ya kutosha kuhakikisha tunafanya vizuri katika mechi ijayo dhidi ya Kagare Sugar," alisema.

"Utakuwa mchezo wa ushindani kwa sababu katika mechi mbili hatujapata ushindi, tunaendelea kujiimarisha kuelekea mchezo wetu dhidi ya Kagera Sugar."

Wakati huo huo uongozi wa timu hiyo, kupitia Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez alisema mbali na ndani ya uwanja klabu hiyo wanakutana na vita kubwa nje na kupambana kuishinda.

Kauli hiyo ni baada ya kukili ukweli wa kufunguliwa mashtaka na ofisa mmoja wa TFF, Jacqueline Kimwemu kwa madai ya kumtolea lugha chafu.

Alisema ameshtusha na taarifa hizo baada ya kupokea barua siku ya Alhamisi iliyopita na kuweka ndani kwa madai hayo, jambo ambalo ana amini ni vita katika soka.

# *Nabi aeleza siri ushindi wa Yanga*

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Asema mechi ilikuwa ngumu, uwanja haukuwa rafiki, Polisi ni timu nzuri, walicheza vizuri na...

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema kuwa na wachezaji wazoefu na wenye vipaji binafsi, uwezo wa kuuchezea mpira ndiyo siri ya ushindi wa mechi dhidi ya Polisi Tanzania na zingine kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha baada ya kumalizika kwa mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, timu yake ikishinda bao 1-0 dhidi ya wenyeji Polisi, Nabi alisema anajivunia kuwa na wachezaji wenye uwezo mkubwa kiuchezaji, uzoefu na vipaji, lakini wamekuwa wakijituma na kuipambania timu kwa sababu wana mapenzi ya dhati ya klabu hiyo.

Kocha huyo raia wa Tunisia alikiri kuwa mechi dhidi ya Polisi Tanzania ilikuwa ngumu, lakini alichofanya wakati wa mapumziko ni kwamba wakapambane na kuongeza nguvu zaidi na wakapata bao moja.

> **"Mechi ilikuwa ngumu, uwanja haukuwa rafiki sana, Polisi ni timu nzuri na walicheza vizuri, ndiyo maana kipindi cha pili niliwaambia wachezaji wangu wapambane na kuongeza nguvu zaidi," alisema Nabi.**

"Kwa kweli nawashukuru wachezaji wangu walifanya nilichowaambia. Unajua timu hii tuna wachezaji wazoefu, wenye vipaji, walio na uwezo wa kuuchezea mpira watakavyo, pia ni wapambanaji na wanaojituma, na hii ndiyo siri ya ushindi kwenye mechi hii, zilizopita na zijazo kwa sababu tuna mikakati fulani msimu huu lazima tuikamilishe."

Kocha huyo alisema kuwa kwa sasa itawalazimu kupambana na timu yoyote kubwa, au ndogo kwenye mazingira yoyote ya uwanja kwa sababu ndiyo ukweli wenyewe halisi na hawawezi kuukwepa.

"Kwa sasa inatulazimu tuwe wazoefu kwenye viwanja vya aina zote, ndiyo ukweli ambao upo na nimeshawaambia wachezaji wangu kuwa kwetu kila mechi ni fainali na hatupaswi kuidharau timu yoyote, iwe kubwa au ndogo, tutacheza kwa kiwango kile kile," alisema.

Naye msemaji wa Polisi, Hassan Juma alisema kuwa walifanya kosa moja ambalo liliwagharimu.

"Ni kama Yanga wamebahatisha hivi, kosa moja tulilofanya ndilo lililowapa bao, lakini ukweli ni kwamba tuliwadhibiti na hawakucheza ule mpira wao wa kawaida tuliouzoea," alisema.

Ilikuwa ni mechi ya tatu kwa Polisi kufungwa msimu huu, ikichapwa idadi kama hiyo ya bao dhidi ya Simba na Coastal Union.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >